

**UDHIRIKAJI WA KANUNI YA DAHL KATIKA LUGHA YA
EKEGUSII**

NA

NYATICHI G. MAKINI

**TASNIFU HII IMEANDIKWA KWA MADHUMUNI YA
KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI
KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

JANUARI, 2015

UNGAMO

Utafiti huu ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada

katika chuo kikuu chochote kwa madhumuni ya kutahiniwa.

Sahihi_____Tarehe_____

GEORGINAH NYATICHI MAKINI

C50/CE/21208/2012

Utafiti huu umewasilishwa katika Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa idhini yetu
kama wasimamizi.

Sahihi_____Tarehe_____

PROFESA IRERI MBAABU

Na

Sahihi_____Tarehe_____

DKT. LEONALD CHACHA

IKISIRI

Utafiti huu ulidhamiria kuonyesha **udhihirikaji wa kanuni ya Dahl** katika viwango mbalimbali pamoja na nomino, vitenzi na maneno ya mkopo. Katika kueleza kanuni ya Dahl, utafiti uliongozwa na malengo yafuatayo: Kueleza jinsi kanuni ya Dahl inavyojidhihirisha katika lugha ya Ekegusii, kuonyesha namna maneno ya mkopo yanavyodhihirisha kanuni ya Dahl kwa kuzingatia lugha ya Ekegusii, kubainisha sifa za kisinkronia na kidaikronia katika Ekegusii. Ili kufanikisha kazi hii, mihimili minne ya nadharia ya Umbo Upeo iliongoza utafiti huu nayo ni; Umajumui, ukiukwaji, upangiliaji masharti zuizi na usambamba. Data msingi ya utafiti ilikusanywa kupitia mbinu ya mahojiano na kusikiliza matamshi katika nyanja mbalimbali. Data iliyokusanywa ilirekodiwa na kuchanganuliwa kwa kuzingatia maswali ya utafiti, malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia ya Umbo Upeo. Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo na majedwali. Matokeo ya utafiti yalibaini kuwa kanuni ya Dahl hujidhihirisha katika nomino, vitenzi na maneno mkopo katika lugha ya Ekegusii. Aidha, utafiti ulionyesha kuwa kupitia kwa tabdila na kuambisha vitenzi vya Ekegusii Kanuni ya Dahl huwezeshwa kujidhihirisha. Utafiti huu uliazimia kuwafaa wasomi wa Kiswahili na isimu za lugha za Kiafrika kwa ujumla kwa sababu, utakuwa na mchango zaidi wa tafiti ambazo zinaweza kurejelewa katika siku za usoni.

ABSTRACT

This study endeavored to investigate **Dahl's Law** in reference with nouns, verbs and borrowed words in Ekegusii. The research intended to accomplish this by realizing the following three objectives; to explain Dahl's Law as revealed in Ekegusii, to illustrate how borrowed words in Ekegusii reveal Dahl's Law, to examine diachronic and synchronic versions of Ekegusii and their characteristics. The research was based on the Optimality Theory (OT) that was postulated by Prince and Smolensky (1993). The study was guided by the following tenets: Principle of universality (constraints are universal and universally present in every grammar), IDENT-10 (input and output must agree on voicing), VOICED-CODA (consonants must not be voiced in coda position) and lastly CONSTRAINT (the set of constraints out of which grammar can be constructed). The theory supposes that there are no language specific restrictions on the input. Every grammar can handle every possible input. Data that was used in this study was collected both in the library and in the field. Collected data was recorded and analyzed based on research objectives, questions and tenets of the theory. Research findings were presented descriptively in five chapters. The study found out that Dahl's Law can be manifested in Ekegusii language by the use of nouns, verbs and borrowed words. The findings of this study will be used as reference in the study of African languages.

SHUKRANI

Nashukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia neema na afya mpaka nilipoikamilisha kazi hii. Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa kunikuza na kunipa fursa ya kutangamana na jamii adhimu tangu nilipoanza shahada hii. Isitoshe, naishukuru sana Idara ya Kiswahili kwa kunilea na kuniweka mikononi mwa Daktari Chacha na Profesa Mbaabu walionishika mkono na kunielekeza katika ulimwengu huu wa kitaaluma. Kila mara wasomi hawa walinipa moyo na kunishajiisha niendeleo na kazi.

Nawashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta: Profesa Mbaabu, Profesa Kinge'i, Profesa Ndungo, Daktari Chacha, Daktari Mwihi, Daktari Masinde, Daktari Wafula, Daktari Ngugi, Daktari Osore na Dkt. Gakuo. Mlinifunza, mkaniongoza na mkanihimiza katika kazi hii. Mungu awabariki wanafunzi wenzangu: Ombese, Moureen, Carol na Mureithi kwa kuwa mlishirikiana nami katika kazi hii. Kuwepo kwenu kulichangia sana katika ufanisi wa masomo yangu.

Nakushukuru mume wangu mpendwa Bw. Caleb Nyangaresi, pamoja na watoto wetu; Esther, Elias, na Elsie kwa kunihimiza na kunisaidia kwa hali na mali nilipokuwa nikisoma. Shukrani za dhati ziwaendee wazazi wangu wapendwa, marehemu babangu Michael Makini na mamangu Teresia Kemunto.

TABARUKU

Mume wangu mpendwa na watoto wetu; Esther, Elias na Elsie

Mungu awabariki sana.

MAELEZO YA ISTILAHU

- Kanuni ya Dahl:** Kanuni ya lugha iliyogunduliwa na Dahl kuhusu lugha ya Kibantu ambapo ikiwa kuna mfuatano wa konsonanti mbili konsonanti mbili zisoghuna zote basi moja hufanywa kuwa ghuna.
- Ukopaji:** Kitendo cha kuhamisha kipashio fulani kutoka lugha moja na kukiingiza katika lugha nyingine.
- Usigano:** Kutofautiana kwa sauti ambazo hapo awali zilikuwa zinafanana kwa kiasi fulani.
- Mofosintaksia:** Ni taaluma ya isimu inayoshughulikia uchanganuzi na uanishaji wa uhusiano uliopo baina ya mofolojia na sintaksia.
- Maumboshindani:** Maumbo mawili au zaidi yanayotaka kupata ukubalifu au upeo.
- Umboghafi:** Maumbo asilia yanayoshindania upeo katika nadharia ya Umbo Upeo
- Umbotokeo:** Umbo lisilovunja sharti lolote au lililovunja masharti yaliyovumilika. Umbo lililopewa ushindi
- Patana:** Kubaliana na masharti


Shabi-SI	Shartizuizi la sifa.
Kidaikronia	Tawi hili huchunguza zaidi mabadiliko yanayotokea katika lugha kwa vipindi mbalimbali vya historia ya lugha hiyo.
Kisinkronia	Tawi hili huchunguza vipengele vya lugha jinsi vilivyo wakati huo bila kuangalia huko nyuma vilivyokuwa.

VIFUPISHO NA ALAMA

*	Mshindani akifanya vibaya
*!	Ukiukaji mkubwa
**	Mshindani akifanya vibaya zaidi
*KYK	Kiyeyusho hakiwezi kutokea katikati ya konsonanti mbili
//	Uwasilishaji wa fonimu
[]	Uwakilishi wa kifonetiki
EABVD	East Africa Bantu Voicing Dissimilation
FIKI-UKO	Fikia Ukomo
HKODA	Silabi haiwezi kuishia na koda
K +GHK-GH	Mfuatano wa konsonanti moja ghuna na nyingine isoghuna
KK+GH	Mfuatano wa konsonanti mbili ghuna
KK-GH	Mfuatano wa konsonanti mbili zisoghuna
KRMF	Kiungo Rasmi cha Fonolojia Mizani
KV	Konsonanti-Vokali
KVK	Konsonanti Vokali Konsonanti
MASHA-ZU	Masharti- zuizi

/

Mazingira ya kifonetiki



Mchakato

NK

Nazali-Konsonanti

OCF

Kanuni Umbo shurutishi

OT

Optimality Theory

SCTD

Nadharia ya mnasaba dhahiri ya usigano

SPE

Sound Patterns of English

TATHI

Tathmin

TEGE-

Tegemeo

UU

Umbo Upeo

V

Vokali

ZALI

Zalishi

Σ

Umbo la silabi

YALIYOMO

UNGAMO	ii
IKISIRI	iii
ABSTRACT	iv
SHUKRANI	v
TABARUKU	vi
MAELEZO YA ISTILAHU.....	vii
VIFUPISHO NA ALAMA	ix
YALIYOMO	xi
ORODHA YA VIELELEZO.....	xv
ORODHA YA MAJEDWALI.....	xvi
SURA YA KWANZA: UTANGULIZI	1
1.0 Usuli wa Utafiti.....	1
1.2 Maswali ya Utafiti.....	6
1.3 Malengo ya Utafiti	6
1.4 Sababu za Kuchagua Mada.....	6
1.5 Upeo na Mipaka.....	7
1.6 Yaliyoandikwa kuhusu Mada	9
1.7 Misingi ya Nadharia.....	15
1.7.1 Nadharia ya Umbo Upeo (UU).....	15
1.7.1.1 Msingi wa kwanza: ZALI.....	16
1.7.1.2 Msingi wa pili: Mashartizuizi: MASHA-ZU	17
1.7.1.3 Msingi wa tatu: Tathmini: TATHI.....	17
1.7.2 Mihimili ya Nadharia.....	17
1.7.2.1 Umajumui	18
1.7.2.2 Ukiukwaji.....	18

1.7.2.3 Upangiliaji.....	18
1.7.2.4 Usambamba.....	19
1.8 Mbinu za Utafiti.....	21
1.8.1 Muundo wa Utafiti.....	21
1.8.2 Mahali pa Utafiti	21
1.8.3 Usampulishaji	22
1.8.4 Vifaa vya Utafiti	22
1.8.5 Mbinu za Kukusanyia Data.....	23
1.8.5.1 Mahojiano	23
1.8.5.2 Usikilizaji wa Matamshi	23
1.8.6 Uchanganuzi wa Data	24
1.8.7 Uwasilishaji wa Matokeo.....	24
1.9 Hitimisho	25
SURA YA PILI: KANUNI YA DAHL KATIKA NOMINO NA VITENZI.	26
2.0 Utangulizi	26
2.1 Fonimu za Ekegusii.....	26
2.1.1 Konsonanti za Ekegusii.....	27
2.1.2 Vokali za Ekegusii	30
2.2 Silabi za Ekegusii.....	34
2.3 Nomino za Ekegusii.....	35
2.3.1 Mofolojia ya Nomino za Ekegusii	35
2.3.2 Ngeli katika lugha ya Ekegusii	37
2.4 Kanuni ya Dahl	38
2.4.1 Mashartizuizi ya Kanuni ya Dahl	41
2.4.2 Familia ya Mashartizuizi ya Uadilifu	42
2.4.3 Familia ya Mashartizuizi ya Uziada	45
2.5 Kanuni ya Dahl katika Nomino za Ekegusii.....	47

2.5.1 Konsonanti ya kiambishi awali ghuna inayofuatwa na kiambishi cha	47
2.5.2 Konsonanti ya kiambishi awali sikhuna ikifuatwa na kiambishi cha kwanza cha mzizi ghuna	49
2.6 Vitenzi vya Ekegusii	54
2.7 Kanuni ya Dahl katika Vitenzi.....	55
2.7.1 Konsonanti ya kiambishi awali ghuna na kiambishi cha kwanza cha mzizi sikhuna.....	56
2.7.2 Konsonanti ya kiambishi awali sikhuna na kiambishi cha kwanza cha.....	57
2.8 Usigano katika sauti za Nazali	61
2.9 Hitimisho	61
SURA YA TATU: MANENO MKOPO NA UDUNISHAJI.....	63
3.0 Utangulizi	63
3.1 Maneno mkopo	63
3.2 Maneno mkopo ya Ekegusii na Kanuni ya Dahl	66
3.2.1 Ngeli ya 12 (udogo)	67
3.2.2 Ngeli ya 7/8.....	71
3.2.3 Ngeli ya 10/11	72
3.6 Hitimisho	73
SURA YA NNE: MTAZAMO WA KIDAIKRONIA NA KISINKRONIA KATIKA EKEGUSII.....	75
4.0 Utangulizi	75
4.1 Uchunguzi wa Kidaikronia	76
4.2 Uchunguzi wa Kisinkronia	78
4.3 Tabdila na nadharia ya Umbo Upeo	79
4.4 Mtindo wa kutumika kwingi wa viambishi	82
4.5 Mashartizuizi na Kanuni ya Dahl katika viambishi tamati.....	84
4.6 Hitimisho	86

SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	87
5.1 Utangulizi	87
5.2 Muhtasari	87
5.3 Matokeo ya Utafiti	89
5.4 Mchango wa Utafiti	91
5.5 Changamoto	91
5.6 Mapendekezo	92
5.7 Hitimisho	93
MAREJELEO	94
KIAMBATISHO A: Kiongozi cha Mahojiano.....	98
KIAMBATISHO B: Orodha ya maneno yaliyoonyesha udhihirikaji wa kanuni ya Dahl.....	99

ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo 2.1: Aina za Konsonanti.....	29
Kielelezo 2.2: Sifa za Vokali za Ekegusii.....	31
Kielelezo 2.3: Vokali Sahili.....	32
Kielelezo 2.4: Muundo wa Silabi.....	34
Kielelezo 2.5: Muundo wa Nomino za Ekegusii.....	36
Kielelezo 2.6: Muundo wa kitenzi Arifu cha Ekegusii.....	54
Kielelezo 2.7: Muundo wa kitenzi cha Kiswahili.....	55

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 2.1: Konsonanti za Ekegusii.....	28
Jedwali 2.2: Kutambua Vokali.....	32
Jedwali 2.3: Orodha ya ngeli za Ekegusii.....	37
Jedwali 2.4: Kanuni ya Dahl na Mashartizuizi.....	46
Jedwali 2.5: Muundo wa Nomino na mabadiliko ya Kanuni ya Dahl.....	48
Jedwali 2.6: Mzizi wa vokali na mabadiliko ya kanuni ya Dahl.....	49
Jedwali 2.7: Viambishi ngeli vinavyodhihirisha Kanuni ya Dahl.....	51
Jedwali 2.8: Nomino na mashartizuizi ya nadharia ya Umbo Upeo.....	53
Jedwali 2.9: Muundo wa vitenzi na mabadiliko ya kanuni ya Dahl.....	56
Jedwali 2.10: Kanuni ya Dahl na mashartizuizi katika vitenzi.....	59
Jedwali 2.11: Vitenzi na mashartizuizi ya nadharia ya Umbo Upeo.....	60
Jedwali 3.1: Mashartizuizi na maneno mkopo ya utohozi.....	70
Jedwali 3.2: Maneno Mkopo na Mashartizuizi ya Nadharia ya Umbo Upeo.....	72
Jedwali 4.1: Tabdila na nadharia ya Umbo Upeo.....	81
Jedwali 4.2: Mtindo wa kutumika kwingi na mashartizuizi.....	84
Jedwali 4.3: Kanuni ya Dahl na Mashartizuizi katika Viambishi tamati.....	85

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.0 Usuli wa Utafiti

Cammenga (2002) anasema, Ekegusii ni lugha ya Kibantu ambayo huzungumzwa na watu takribani milioni moja na nusu Kusini Magharibi mwa Kenya. Guthrie (1967) aliorodhesha lugha hii katika kundi la “E35”. Majina mengine yanayotambulisha lugha hii ni kama Guz, Kisii, Gusii na Ekegusii. Jina la Ekegusii litatumika katika kazi hii. Wakisii walihama kutoka Afrika ya Kati kupitia Mlima Masaba ambao kwa leo hujulikana kama Mlima Elgon. Walihamia kusini magharibi mwa Kenya ambako wanapakana na Wakalenjini na Wamasai. Kama familia ya lugha za Kibantu, Ekegusii kina vigezo vya Ubuntu kama vile kimsamiati, kifonolojia, kimofolojia na unyambulishaji.

Msamiati wake wa kiasili unakurubiana na lugha zingine za Kibantu. Kimofolojia, maumbo ya maneno yake ni kama ya lugha zingine za Kibantu. Maumbo ya maneno yanafuata utaratibu wa kuambishwa viambishi. Aidha, mfumo wa sauti katika lugha hii unadhihirisha Ubuntu kwa kuwa silabi zake zote ni wazi. Hakuna silabi funge yaani inayoishia na konsonanti.

Guthrie (1967) anasema kuwa kuna uafiki wa kijumla kwamba lugha nyingi ulimwenguni hupendelea silabi yenye muundo wa konsonanti vokali. Kwa hivyo, mpangilio wa konsonanti vokali (KV) ni umbo bia la silabi (Schane 1973; Hyman 1975). Hata hivyo, maumbo ya silabi hutegemea lugha inayohusika. Lugha ya Ekegusii ina maumbo mbalimbali ya silabi. Hivi ni kusema kwamba silabi za lugha ya Ekegusii huishia katika sauti za vokali na zingine huishia kwa sauti za konsonanti. Umbo la KV ndilo hutumika kwa wingi katika maneno ya lugha ya Ekegusii.

Kwa kushadidia ukweli huu, silabi za KV hutumika katika mazingira yote ya kifonetiki; mwanzo, ndani na tamati kama inavyodhihirika katika maneno: *rika* (andika) na *tara* (tembea). Kila moja ya maneno haya inajumuisha silabi mbili za KV. Silabi zinapounganishwa huunda aina mbalimbali za maneno kama vile; nomino, vitenzi, vivumishi, vielezi na viunganishi.

Vitenzi ni maneno yanayosimamia kitendo. Kila kitenzi huwa na shina yaani, sehemu ndogo zaidi ya kitenzi ambayo ndiyo huwakilisha tendo hilo. Dhima ya kitenzi ni kueleza na kuarifu jambo fulani linalohusu kiima cha sentensi. Lugha ya Kiswahili ina mahusiano ya karibu na lugha ya Ekegusii katika vipengele mbalimbali. Hivi ni pamoja na taratibu za uambishaji na unyambulishaji. Kwa mfano;

(1) a. m-tu wa-tu (Kiswahili)

b. o-mo-nto a-ba-nto (Ekegusii)

Kuna viambishi vinavyotoa maana ya mtendaji, wakati, mzizi na pia kauli ya kitendo hicho. Haya yote yanathibitisha kuwa Ekegusii ni mojawapo wa lugha za Kibantu. Katika lugha ya Ekegusii kuna uwezekano wa kuunda nomino kutokana na vitenzi, kuunda vitenzi kutokana na nomino, kuunda vitenzi kutokana na vivumishi, na pia kuunda majina kutokana na vivumishi, kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo;

(2) Kitenzi	Jina	Jina	Kitenzi
a. tera	ogotera	omorugi	ruga (Ekegusii)
b. imba	wimbo	mpishi	pika (Kiswahili)

Mada hii inapatikana katika eneo pana la fonolojia. Sauti zinapotumiwa pamoja katika maneno huweza kuathiriana na zikapata sifa mpya za kifonetiki. Harakati zinazosababisha hali hii huitwa mifanyiko ya kifonolojia ambayo husababisha mabadiliko ya kifonolojia. Mifanyiko hii haishughulikii vipande sauti bali maumbo dhahiri katika makundi mahsusi. Makundi haya yanaweza kuwa sehemu ndogo ya silabi au kubwa kama umbo la kutamkika. Sifa moja kuu ya lugha za Kibantu ni kuambatisha na hupendelea muundo wa silabi wazi hasa KV. Mofimu zinapounganika huathiri vipande vilivyokuja pamoja na hata utaratibu wa kiimbo.

Massamba na wenzake (2003) wanasema kuwa katika kiwango cha kifonolojia mofimu mbili zinapokutanishwa kuna mambo mawili yanayoweza kutokea. Ama kugotana huku kunaweza kuleta mabadiliko katika kimoja kati ya vipandesauti vinavyohusika au kutakuwa hakuna badiliko lolote. Michakato hii ni ya aina mbili; kuna ile inayotokana na usilimisho na ile isiyotokana na usilimisho. Michakato ya usilimisho ni; unazalishaji wa irabu, utamkiaji pamwe nazali, ukaakaishaji, ughunishaji katiirabu, uhafifishaji katiirabu, tangamano katiirabu, ughunishaji ifuatayo; nazali, mvuto wa irabu, tangamano la irabu na kudondoshwa kwa irabu na muungano. Michakato isousilimisho ni kama vile: udondoshaji kati, tabdili, uchopezi usomwanzo na uchopezi mwanzo.

Utafiti huu utaangazia aina moja ya mifanyiko hii ya kifonolojia ambayo ni usigano katika Ekegusii. Usigano ni kutofautiana kwa vitamkwa ambavyo hapo awali vilikuwa vikifanana ili kufanya sauti hizi mbili kutofautishwa. Kanuni ya Dahl hutumika kueleza swala hili la usigano. Kanuni ya Dahl ni kanuni ya lugha iliyogunduliwa na Dahl kuhusu lugha za Kibantu ambapo ikiwa kuna konsonanti mbili ghuna moja hupoteza ughuna wake, au kama kuna mfuatano wa konsonanti mbili zisoghuna moja hufanywa ghuna. Kazi hii itaangazia kanuni ya Dahl inavyodhihirika katika lugha ya Ekegusii.

1.1 Swala la Utafiti

Usigano hujidhihirisha kwenye konsonanti katika lugha nyingi za Kibantu hasa katika upwa wa Afrika Mashariki. Kanuni hii ya Dahl imezungumziwa na wataalamu mbalimbali kama vile Kaimenyi (2002), Davy na Nurse (1982), Bickmore (1998), Bennett na Sharon (2004) kuhusu lugha tofauti hata pamoja na lugha ya Ekegusii. Davy na Nurse (1982) wameainisha sifa za usigano za kidaikronia na kisinkronia wakiwa wanazingatia sheria ya usigano katika lugha za Kibantu za Afrika Mashariki (EABVD). Wataalamu hawa wameonyesha mitindo tofauti ya kidaikronia na kisinkronia. Kisinkronia, utafiti wao umeonyesha sauti /k/ kubadilika katika mzizi na kuwa /g/ bila kubainisha makundi ya maneno hayo. Utafiti huu utaweka wazi mabadiliko ya kidaikronia na kisinkronia kwa kuzingatia sheria ya usigano ambayo inabadilika kutoka /k/ kwenda kwa /g/ huku ikionyesha wazi aina za maneno kama vile; nomino na vitenzi. Aidha, utafiti utaonyesha jinsi sauti /nk/ inavyobadilika kwenda kwa /ng/ pamoja na maneno mengine yaliyotumika kidaikronia ambayo hayakushughulikiwa na Davy na Nurse. Bickmore (1998) ameonyesha kuwa kanuni hii hujidhihirisha tu katika vitenzi lakini utafiti huu utaeleza zaidi kuhusu nomino, vitenzi na maneno ya mkopo kwa kuzingatia nadharia ya Umbo Upeo ambayo haikutumika hapo awali na watafiti wengine. Kupitia kwa Kanuni ya Dahl, sarufi ya Ekegusii itachanganuliwa kwa utaratibu, umakini na kwa namna inayoeleweka.

1.2 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu utaongozwa na maswali ya utafiti yafuatayo:

1. Kanuni ya Dahl inajidhihirisha vipi katika Ekegusii kwenye nomino na vitenzi?
2. Katika lugha ya Ekegusii Kanuni ya Dahl inajidhihirisha vipi kwenye maneno mkopo?
3. Usigano una sifa zipi za kisinkronia na kidaikronia katika lugha ya Ekegusii?

1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu utaongozwa na malengo yafuatayo:

1. Kueleza jinsi Kanuni ya Dahl inavyojidhihirisha katika Ekegusii kwenye nomino na vitenzi.
2. Kufafanua namna maneno ya mkopo yanavyodhihirisha Kanuni ya Dahl katika lugha ya Ekegusii.
3. Kubainisha sifa za kisinkronia na kidaikronia katika usigano kwa kuzingatia lugha ya Ekegusii.

1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Kutokana na uchunguzi wa awali wa mtafiti, imebainika kwamba kuna tafiti chache sana za mada hii ya Kanuni ya Dahl katika lugha za Kibantu basi utafiti huu utaweza kuongeza ujuzi zaidi kuhusu dhana hii ya usigano katika lugha ya Ekegusii.

Utafiti huu pia ni muhimu kwa jinsi ambavyo utachangia kwa kuipa lugha ya Ekegusii ukwasi wa istilahi katika nyanja tofauti. Maneno yatakayokusanywa yanaweza kujumulishwa katika matoleo mapya ya maandishi ya Isimu Jumulifu.

Uchunguzi huu ni muhimu kwa wanaisimu wa lugha za Kiafrika hasa za Kibantu. Data inayohusika inaweza kutumika kwa utafiti wa lugha za Kiafrika badala ya kurejelea tahakiki za lugha ya Kiingereza. Utafiti huu pia unaweza kuleta usawasisho katika lugha kukiwa kwamba hakuna lugha bora kuliko nyingine.

Utafiti huu pia utatumiwa kubainisha tofauti zilizopo kati ya lugha ya Ekegusii na lugha nyingine za Kibantu. Kwa hivyo data inayohusika inaweza kuchangia tawi la Isimu Linganishi katika vyuo mbalimbali vya isimu. Matokeo ya utafiti yana umuhimu katika kupanua maarifa kuhusu sarufi ya Ekegusii.

Katika usomi wa Kiswahili na isimu za lugha za Kiafrika kwa jumla kutakuwepo na mchango zaidi wa tafiti ambazo zinaweza kurejelewa katika siku za usoni hasa na wataalamu wa lugha. Uchunguzi huu una nafasi ya kuchangia usomi wa Kiswahili na isimu za lugha za Kiafrika kwa jumla.

1.5 Upeo na Mipaka

Utafiti huu utajikita katika udhihirishaji wa Kanuni ya Dahl katika viwango mbalimbali. Utafiti utachunguza nomino, vitenzi na maneno ya mkopo katika

lugha ya Ekegusii. Katika Kiswahili, nomino ndilo neno linalotawala maneno mengine katika sentensi au kikundi cha maneno na kuathiri muundo wa maneno haya. Katika lugha ya Ekegusii, nomino zimepangwa kwa kuzingatia ngeli mbalimbali. Nomino nyingi za Ekegusii hudhihirisha Kanuni ya Dahl. Utafiti huu hautaangazia aina mbalimbali za nomino katika lugha ya Ekegusii bali mifano ya nomino inayodhihirisha kanuni ya Dahl.

Aidha, Kanuni ya Dahl hudhihirika katika vitenzi vya Ekegusii. Dhima ya kitenzi ni kueleza na kuarifu jambo fulani linalohusu kiima cha sentensi. Utafiti utaonyesha udhihirikaji wa Kanuni ya Dahl kupitia vitenzi vya Ekegusii. Utafiti huu pia utahusu maneno ya mkopo. Maneno ya mkopo ni maneno yaliyotolewa lugha nyingine yakapewa matamshi ya lugha ngeni au lugha ya pili. Utohozi huu husababisha mabadiliko kwa aina mbalimbali ya maneno. Chanzo cha mabadiliko huwa mahitaji ya ukuaji wa lugha kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine mtagusano wa lugha. Mtagusano wa lugha husababishwa na mahusiano ya kijamii kama vile shughuli za kibiashara au maingiliano ya kitamaduni. Maneno yanapokopwa kutoka kwa lugha ya Ekegusii kwenda kwa lugha ya Kiswahili huathiriwa na Kanuni ya Dahl. Kiambishi awali katika Ekegusii kinapokopwa kwa lugha ya Kiswahili hudhihirisha Kanuni ya Dahl. Kwa mfano;

(3) Ekegusii Kiswahili

a. ege-kombe ki-kombe

b. ege-tabu ki –tabu

Ukopaji huu pia huathiri maneno yanapokopwa kutoka kwa lugha ya Kiingereza kwenda kwa lugha ya Ekegusii. Aidha, sifa za kidaikronia na kisinkronia zitawekwa wazi kwa lugha ya Ekegusii pasina kuangalia lugha nyingine. Lugha ya Ekegusii ni lugha ya toni lakini utafiti huu hautazingatia kwa kuwa haliathiri usigano.

1.6 Yaliyoandikwa kuhusu Mada

Uchunguzi huu umezingatia maandishi kuhusu udhihirikaji wa Kanuni ya Dahl. Maandishi ya kijumla kuhusu kanuni ya Dahl yameelezwa na wataalamu wengi. Kanuni ya Dahl ilipata jina kutokana na mwanzilishi wake kwa jina Edmund Dahl. Kanuni hii ilielezwa zaidi na Meinhof ambaye alisema kuwa sauti /k/ huwa ghuna katika mazingira ya konsonanti isoghuna. Meinhof (1932) anasema kuwa kanuni hii inahitaji konsonanti ya kiambishi awali kutofautiana kisauti na konsonanti ya mzizi inayoambatanishwa nayo.

Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha (1990) inasema kuwa Kanuni ya Dahl ni kanuni ya lugha iliyogunduliwa na Dahl kuhusu lugha ya Kibantu ambapo ikiwa kuna mfuatano wa konsonanti mbili ghuna moja hupoteza ughuna wake, au kama

kuna mfuatano wa konsonanti mbili zisoghuna basi moja hufanywa kuwa ghuna. Armstrong (1967) anasema, Kanuni ya Dahl katika lugha za Kibantu ni utaratibu wa kihistoria ambapo kiambishi awali kikiwa /g/ silabi inayofuata sharti iwe soghuna na iwapo kiambishi awali kimeanza na /k/ ni lazima sauti inayofuata iwe ghuna. Pindi tu viambishi pamoja na mzizi vinavyotii kanuni hii, ndivyo kiambishi awali hutofautiana kisauti na kiambishi kinachofuata.

Katamba (1989) anasema kuwa mzizi ulio na kipande kilicho ghuna huhitaji konsonanti isoghuna katika kiambishi awali na mzizi ulio na kipande kisicho ghuna huhitaji konsonanti ghuna katika kiambishi awali. Kanuni hii hujidhihirisha katika mipaka yote ya fonimu.

Bennett na Sharon (2004) walitafiti Thetogovela Molo, lugha ya Kordofania ya Sudan. Katika utafiti wao, hawakutumia kanuni za usigano ambazo ni Kanuni ya Umbo Shurutishi (OCP) na enye uziada yaani iliyo na sifa zaidi kuliko nyingine. Wao walichunguza usigano kwa kutumia kanuni ya Bennett (2013) ambayo ni nadharia ya mnasaba dhahiri ya usigano (SCTD). Nadharia hii husisitiza makubaliano kwa mnasaba.

Lombardi (1991) ametafiti lugha ya Kikuyu ambapo anasema kuwa uchanganuzi wa Kanuni ya Dahl unakuwa rahisi kueleweka kwa kutumia uchanganuzi wa fonolojia vipandesauti huru ambao husisitiza uambatanishaji wa sehemu nyingi.

Anaeleza Kanuni ya Dahl kama matokeo ya Kanuni ya Umbo Shurutishi (OCP) kwa sauti baina ya kiambishi awali kwa mkururo wa sauti. Japo hivyo, kiambishi kinachofuata mkururo wa sauti huepuka athari ya Kanuni ya Umbo shurutishi (OCP). Ni dhahiri kuwa kuambatanisha sehemu nyingi ni jambo la lazima katika uchanganuzi huu. Jambo hili la kuambatanisha sehemu nyingi za viambishi awali huonyesha kuwa kuna sheria nyingine ya kuenea. Uenezi huu hufikia kikomo iwapo utakiuka matokeo ya kanuni ya Umbo shurutishi (OCP). Katika lugha ya Ekegusii, utafiti huu utaangalia lugha kisinkronia lakini hautaangazia matokeo ya Kanuni Umbo Shurutishi.

Kaimenyi (2002) alitafiti lugha ya Kinyarwanda ambapo alisema kwamba Kanuni ya Dahl ni usigano wa sauti ambao unafanya konsonanti isoghuna kuwa ghuna kabla ya mzizi wa neno ambao una konsonanti isoghuna. Utaratibu huu hupatikana katika maneno ya mkopo, vihisishi na maneno yanayoiga sauti. Kanuni hii huathiri viambishi awali, viambishi viwakilishi wakati na viwakilishi. Kulingana na data aliyokusanya, kanuni hii pia hujidhihirisha katika viambishi tamati hasa katika vitenzi kwa kuwa vitenzi ndivyo huchukua viambishi. Aidha, kanuni hii hudhihirika katika maneno mkopo lakini si katika viambishi awali na viambishi tamati bali ndani ya mzizi wenyewe. Maneno mkopo yaliyo na silabi funge hupewa vokali ili neno liwe na silabi wazi. Utafiti huu utaonyesha udhihirikaji wa kanuni ya Dahl katika nomino, vitenzi na maneno mkopo.

Kithaka wa Mberia (1981) ametafiti lugha ya Kitharaka kwa kuzingatia mifanyiko ya konsonanti za nazali kama vile; usilimisho wa vitamkwa pamwe vya nazali, ukaakaishaji wa nazali na usigano wa nazali. Lugha ya Kitharaka hudhihirisha Kanuni ya Dahl. Kuna ushahidi wa kutosha kutoka Kitharaka kuwa Kanuni ya Dahl huwekewa sharti na konsonanti isoghuna. Kanuni hii pia hujidhihirisha wakati konsonanti ya kwanza inayofuata konsonanti ya kaaka laini ni konsonanti ya nazali. Konsonanti za nazali huchangia udhihirikaji wa Kanuni ya Dahl. Utafiti wetu hautaangazia mifanyiko mbalimbali ya konsonanti katika Ekegusii.

Kanana (2011) ametafiti juu ya kanuni hii katika lahaja ya Chuka na Imenti. Kifonolojia, lahaja hizi mbili zinapokaribiana sana huwa na mfumo wa vokali unaofanana na zina mfumo wa vokali saba unaojumulisha vokali fupi na vokali ndefu. Kulingana na masharti ya mofofonolojia, mifanyiko mbalimbali ya vokali hujidhihirisha katika lahaja hizi kama vile uumbaji wa viyeyusho, urefushaji wa usilimisho na muungano. Lahaja hizi hazina mfumo unaofanana na ule wa konsonanti kama ule utaratibu unaopatikana katika vokali. Kuna matokeo ya kisinkronia kwa lahaja zote. Utafiti huu ni tofauti kwa kuwa utajikita katika lugha ya Ekegusii bila kuangalia mifanyiko ya vokali.

Bickmore (1998) amejadili kanuni ya Dahl katika lugha ya Ekegusii kwa kuzingatia mifano ya vitenzi bila kuangazia mifano mingine ya maneno. Aidha, amezungumzia mabadiliko ya kisinkronia na kidaikronia. Anaamini kuwa data ya

kisinkronia inasababisha mabadiliko ya kidaikronia ambayo yanaathiri konsonanti mbili, ya kwanza huwa ni sauti ya kaaka laini inayofuatwa na vokali. Bickmore anaonyesha kuwa utaratibu huu hutokea tu panapokuwa na konsonanti ya midomo ambayo inafuata sauti ghuna katika neno. Usigano huu hutokana na utaratibu wa utoaji sauti unaopatikana katika lugha nyingi za Kibantu unaojulikana kama Kanuni ya Dahl. Katika uchanganuzi wake Bickmore hakupanga maneno yaliyoanza kwa konsonanti sikhuna na hivyo kusababisha konsonanti ya mzizi kuwa ghuna. Aidha, hakuonyesha kiambishi awali kikiwa ghuna na hivyo konsonanti ya mzizi kuwa sikhuna. Vilvile, uchunguzi wake haukueleza jinsi kategoria mbalimbali za maneno zinavyoathiriwa na kanuni hii. Utafiti huu utaeleza namna kategoria mbalimbali za maneno kama vile vitenzi, nomino na maneno ya mkopo yanavyopitia mabadiliko hayo.

Davy na Nurse (1982) waliweza kutofautisha mitindo mbalimbali ya kidaikronia na kisinkronia. Kidaikronia, utaratibu huu umeathiri sauti /k/ kwa kila lugha ambapo inaacha mzizi ukibadilika kwenda kwa /g/. Katika Kimeru, Kikisii na Kikuria kanuni hii imeathiri sauti ya /nk/ ikibadilika na kuwa /ng/ kwenye mizizi mingi inayoonekana. Kwa mfano, katika Ekegusii huathiri konsonanti ya kwanza kwenye mzizi na kusababisha ibadilike kuwa /g/

(4) [a-ka-goko] - kuku mdogo

Mfano wa [aka-goko] huonyesha utaratibu wa kisinkronia ambapo sauti /g/ huwa katika mizizi. Japo utaratibu huu unaosababishwa na usigano wa sauti /k/ hauleti mabadiliko ya kisinkronia kwa viambishi awali kwa lugha za Kibantu za Afrika Mashariki. Kigezo kimoja kinachotawala utaratibu huu ni urefushaji wa kitenzi kwa kuongeza irabu. Hali hii husababisha utamkaji wa haraka au wa polepole.

Masharti ya kisinkronia ya viambishi awali huhitaji uwezo wa kifonolojia wa kidaikronia unaosababisha konsonanti kuwa ghuna. Kifonolojia, mifano ya kidaikronia inapowakilishwa huleta mifano mipya ya kisinkronia ikiwa na konsonanti za mwanzo zisizo ghuna ambapo zote zilitii masharti pamoja na sehemu zilizopatikana katika mipaka hii ya kimofolojia. Kwa hivyo kisinkronia sauti /k/ hubakia mwanzoni, ama mahali kipande kinachotii masharti kinapopatikana. Kutokana na sharti hili la kisinkronia (EABVD), tunaweza kutarajia /k/ kubadilika kuwa /g/. Kwa hakika lugha nyingi za Kibantu huonyesha vibadala hivi katika viambishi awali. Mabadiliko kwenye lugha hii hujitokeza katika silabi ya mwisho ya mzizi na katika viambishi awali. Davy na Nurse hawakuonyesha mifano hii kwa kuzingatia sifa hii ya kisinkronia. Aidha, mifano mingine ya kihistoria haikudhihirika katika utafiti wao. Utafiti huu utafidia sehemu hizo pamoja na kutoa mifano zaidi inayodhihirisha mabadiliko ya sauti /nk/ kwenda kwa /ng/. Maandishi haya yanaweza kurejelewa katika utafiti huu, lakini tafiti bayana kuhusu Kanuni ya Dahl zinahitajika ili kutoa mwanga zaidi kuhusu mada.

1.7 Misingi ya Nadharia

Mnamo mwaka wa 1993, Alan Prince na Paul Smolensky walipendekeza kiunzi ambacho kinajulikana hii leo kama nadharia ya Umbo Upeo (UU) na kiunzi hiki kikatiwa mwanga baadaye na John J. MacCathy na Alan Prince mnamo mwaka huo wa 1993. Kiuzui hiki cha nadharia ya Umbo Upeo kingali kinaendelezwa na wanaisimu kutoka pembe mbalimbali za ulimwengu wa taaluma. Kumetokea na bado kunaendelea kutokea mapendekezo na mabadiliko mbalimbali kwa hivyo sura yake bado inaendelea kuchongwa. Kutokana na matatizo yaliyojitokeza katika Kiungo Rasmi cha Fonolojia Mizani (KRFM) kuhusu udhahania wa uwakilishaji wa vipengele vya fonolojia, Alan Prince na Paul Smolensky walijaribu kupendekeza kiunzi ambacho, kwa mujibu wa maelezo yao, kiliachana na sheria za ukokotozi na kupunguza udhahania. Madhumuni ya mwanzo kabisa ya kuanzishwa kwa nadharia hii yalikuwa ni kushughulikia masuala ya kifonolojia ambayo yalionekana kujitokeza katika kitabu cha *The Sound Patterns Of English* (1968) (SPE). Hata hivyo, baadaye kimetumiwa pia kushughulikia masuala mengine ya kiisimu kama vile mofolojia na sintaksia. Kiunzi hiki kitatumiwa kufafanua kanuni ya Dahl kwa kuzingatia mfumo kamili wa sarufi ya Ekegusii.

1.7.1 Nadharia ya Umbo Upeo (UU)

Prince na Smolensky (1993) wanaamini kwamba miundo mbalimbali ya lugha hutokana na mkinzano kati ya masharti zuizi yaliyopo. Madai haya yamekitwa

katika imani kwamba tofauti zilizopo kati ya lugha ya binadamu hutokana na tofauti za uthamini wa masharti zuizi yanayohusu mpangilio wa sauti, maneno au hata virai. Nadharia ya UU imejengeka katika misingi mikuu mitatu nayo ni;

- Zalishi (Zali)
- Masharti zuizi (Masha-zu)
- Tathmini (Tathi)

1.7.1.1 Msingi wa kwanza: ZALI

Hiki ni kipengele ambacho huzalisha maumbotokeo mbalimbali katika lugha ambayo kwa hakika tunaweza kuyaita maumboshindani. Tunayaita maumbo shindani kwa sababu katika mambo hayo ndimo tunamopata asili ya jina la upeo kwa ukubalifu. Hapa ndipo tunapata asili ya jina la nadharia hii. Kitu kinachoangaliwa katika nadharia hii ni lile umbo, kati ya maumbotokeo ambayo yote ni maumboshindani. Umbo linaloshinda ndilo linalosemekana kuwa limefikia upeo wa ukubalifu (Prince na Smolensky 1993).

Umbo fulani linapofikia upeo wa ukubalifu huwa hatuna maana kwamba umbo hilo ni lazima halijavunja masharti zuizi yoyote, la hasha. Umbo linaweza kuwa limevunja mashartizuizi kadhaa lakini kwa kuwa mashartizuizi hayo yaliyovunjwa ni ya hadhi ya chini, kwa maana kwamba yanavumilika katika ule utaratibu msonge wa mashartizuizi, litahesabika kuwa ndilo lililofikia upeo wa ukubalifu katika lugha hiyo.

1.7.1.2 Msingi wa pili: Mashartizuizi: MASHA-ZU

Hiki ni kipengele kingine katika nadharia ya UU ambacho kinahusika na uwekaji vigezo na masharti yasiyoweza kuvunjwa na yanayoweza kuvunjwa; vigezo ambavyo ndivyo vitumikavyo katika kuamua ni umbo lipi linafikia upeo wa ukubalifu. MASHA-ZU hufanya kazi na maumbotokeo, kwa maana huyawekea maumbo mashartizuizi. Lile umbotokeo ambalo halikuvunja masharti yoyote au ambalo limevunja masharti yanayovumilika ndilo lipewalo ushindi.

1.7.1.3 Msingi wa tatu: Tathmini: TATHI

Mwisho, kuna kipengele cha TATHI. Hiki ndicho kipengele muhimu sana katika nadharia hii kwa sababu ndicho kinachoamua ni umbo lipi kati ya maumbotokeo yaliyopo limefikia upeo wa ukubalifu. TATHI hufanya hivyo kwa kuangalia ni memba yupi, katika jumla ya washindani huvunja masharti zuizi muhimu mengi, yupi kavunja kidogo na yupi kavunja yale ya chini zaidi.

Nadharia hii ya UU huchukulia kwamba vipengele hivi vitatu hupatikana katika kila lugha ya binadamu. Aidha, nadharia ya UU huchukulia kwamba tofauti zinazojitokeza katika sarufi za lugha mbalimbali za ulimwengu huwa zinaakisi namna tofautitofauti za mpangilio wa seti majumui ya masha-zu.

1.7.2 Mihimili ya Nadharia

Prince na Smolensky (1991) wanasema kwamba nadharia ya Umbo Upeo hufanya kazi kwa kuegemezwa kwenye mihimili mikuu minne ambayo ni;

- Umajumui
- Ukiukwaji
- Upangiliaji masha-zu
- Usambamba

1.7.2.1 Umajumui

Lengo kuu la nadharia yoyote ya kiisimu ni kujaribu kuchunguza na hatimaye kugundua sifa za kimajumui zilizomo katika lugha ya binadamu. Sifa hizo ndizo zilizolenga kitu kiitwacho sarufimajumui. Kwa mujibu wa nadharia ya UU, sarufimajumui ina seti za masha-zu ambayo ni ya kimajumui na yanapatikana katika sarufi zote za lugha ya mwanadamu (McCarthy 2003).

1.7.2.2 Ukiukwaji

Kwa kuwa masharti zuizi ni ya kimajumui, ufuatwaji au ukiukwaji wake hutegemea lugha inayohusika. Kutokana na sharti zuizi utaona kwamba kanuni hii ndiyo inaonekana hafifu katika lugha nyingi.

1.7.2.3 Upangiliaji

Masharti zuizi yote katika masha-zu huwa katika mpangilio msonge unaofuata nguvu na uhafifu wa masharti hayo katika lugha inayohusika. Ukiukwaji wa masharti zuizi huwa ni wa kiwango kidogo tu, kwa hakika huwa tunazingatia mpangilio wa hayo masharti katika lugha mahsusi. Kauli hii pia ina maana kwamba ukiukwaji wa masharti zuizi unapozidi, sarufi ile itakuwa haikubaliki

katika lugha inayohusika. Maumbo tokeo ambayo yanakiuka masharti zuizi ambayo ni hafifu huwa na uwezekano mkubwa zaidi wa kufikia upeo wa ukubalifu kuliko yale maumbo ambayo yanakiuka masharti zuizi yenye nguvu.

1.7.2.4 Usambamba

Utoshelezi wa kimpangilio wa masharti zuizi huangalia kwa kutazama jinsi seti nzima ya maumbo tokeo inavyodhihirika katika mpangilio wote kwa jumla. Nadharia ya UU huchukulia kwamba kila lugha huweza kupokea maumbo ghafi ya aina yoyote. Hali hii inaitwa ukwasi wa chanzo. Yaani kila sarufi ya lugha ya binadamu inaweza kuhimili kuchukua umbo ghafi lolote lile. Hakuna ukomo au masharti katika kupokea maumbo ghafi. Katika lugha ya Kiswahili kwa mfano, kuna umboghafi “mstakabali” ambalo tuseme linatamkwa [mstaka`bali], lakini maumbotokeo yake ni; mustakbli, musta`kabal, musitak`bali, mustakaba`li. Katika maumbotokeo haya tunaona kwamba maneno matatu mwanzo yamechopeka irabu **u** kati ya **m** na **s**, na neno la tatu, mbali na kuchopeka sauti hiyo **u** limechopeka pia sauti **i** katikati ya **s** na **t**.

Lugha ya Ekegusii ni miongoni mwa lugha za Kibantu zinazodhihirisha maneno kidaikronia ukirejelea mifano mbalimbali ya Mame-Bantu. Kiambishi ‘g’ hufuata utaratibu wa gVK na baadaye huwa KVg. Kwa mujibu wa nadharia hii, ikiwa na maumboghafi yoyote yale ZALI huzalisha idadi isioukomo ya maumbotokeo au

maumboshindani kutokana na hayo maumboghafi. Sarufi ya lugha (kulingana na mpangilio wake wa masharti zuizi) ndiyo itakayoamua ni umbo tokeo lipi kati ya idadi hiyo ya maumboshindani litatathminiwa na TATHI kuwa ndilo umbo upeo.

Kager (1991) anasema kuwa katika nadharia ya UU kila shartizuizi lina sifa ya umajumui. Hii ina maana kwamba sifa ya MASHA-ZU ni hiyo hiyo katika kila lugha. Nadharia ya UU hutambua familia za masharti zuizi za aina mbili: Familia ya mashartizuizi ya uadilifu na familia ya mashartizuizi uziada. Familia ya mashartizuizi ya uadilifu huhitaji kwamba umbotokeo kwanza liwe linakubalika katika lugha inayohusika lakini pia lifanane kwa namna fulani na umboghafi lililoingizwa. Hii ina maana kwamba mashartizuizi haya huhitaji pawepo na mshabaha baina ya maumbo ghafi na maumbo yanayozalisha, yaani maumbo tokeo.

Mashartizuizi ya uziada huweka au huondoa alama za ziada katika maumboghafi na kulifanya umbo linalohusika lifikie kilele cha ukubalifu kwa wasemaji wazawa. Mashartizuizi ya utangamano na mashartizuizi ya uziada hutofautiana toka lugha moja hadi nyingine. Mihimili hii ya nadharia ya Umbo Upeo itatumika katika kuchanganua data ya kazi hii.

1.8 Mbinu za Utafiti

Sehemu hii itashughulikia muundo wa utafiti, mahali pa utafiti, sampuli na uteuzi wa sampuli, vifaa, mbinu za kukusanyia data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data.

1.8.1 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu utachukua muundo wa kimaelezo. Utafiti wa kimaelezo ni ule ambao hutegemea maelezo katika uwasilishi na uchanganuzi wake. Mbinu hii itatumika katika utafiti huu kueleza udhihirikaji wa kanuni ya Dahl katika Ekegusii.

1.8.2 Mahali pa Utafiti

Utafiti utafanywa maktabani na nyanjani. Utafiti wa maktabani utazingatia masuala kuhusu Kanuni ya Dahl. Vitabu, tasnifu, majarida, na machapisho yanayohusiana na mada ya utafiti yatapitiwa. Mtandao pia utakuwa wa msaada hasa kwa masuala ya hivi karibuni yanayolenga mada. Utafiti msingi utaelekea kule nyanjani kwa lengo la kukusanya data. Mahojiano na kusikiliza matamshi ni miongoni mwa vifaa vya kukusanya data. Nyanjani, eneo la wilaya ya Kisii Kasikazini, tarafa ya Suneka, kijiji cha Bomwanda litakuwa mahali petu pa utafiti. Eneo hili limechaguliwa kwa sababu hapa ndipo utakutana na wazawa wa lugha hii ambao hasa hawajaathiriwa na lugha nyingine. Pia, eneo hili ni mwafaka kwa sababu halijapakana na miji ili kupata athari ya lugha tofauti.

1.8.3 Usampulishaji

Usampulishaji ni kile kitendo cha kuchagua kitu kimoja kati ya vingi vya aina kikachukuliwa kama mfano mzuri wa vitu hivyo kwa kuviwakilisha. Sampuli ni sehemu ya idadi maalum ya watu ambayo mtafiti ataitumia katika ukusanyaji wa data itakayomsaidia kufikia malengo yake. Utafiti utatumia sampuli kusudi na sampuli ya kinasibu. Kombo na Tromp (2006) wanasema kuwa sampuli kusudi huwa mwafaka pale ambapo kundi fulani linaaminiwa ndilo lina data mwafaka inayoafiki malengo ya utafiti. Sampuli ya kinasibu huwa muhimu ili kutoa nafasi sawa ya ushirikisho wa data na wahojiwa; haina mapendeleo. Wahojiwa wenye umri wa miaka hamsini kwenda juu watateuliwa kwa sababu ya tajriba na uzoefu wa lugha. Mugenda (2003) anaeleza kuwa aghalau asilimia kumi ya walengwa hutosha katika tafiti za kimaelezo. Wahojiwa thelatini watateuliwa watakaotoa data itakayowakilisha lile kundi kubwa la watu. Walengwa watapewa maneno yaliyoteuliwa wayatamke ili kuthibitisha mabadiliko ya viambishi kutoka sikhuna kwenda ghuna au kutoka ghuna kwenda sikhuna.

1.8.4 Vifaa vya Utafiti

Vifaa kama vinasa sauti, kalamu na daftari vitatumika kukusanya data. Maneno yatakayotamkwa yatarekodiwa kwenye daftari tayari kuchanganuliwa. Data itakayokusanywa itarekodiwa kwa kutumia vinasa sauti. Kanda hizi zitakidhi mapungufu yatakayojitokeza kwa kushiriki mahojiano, kwani si rahisi mtafiti kunukuu kila kitu.

1.8.5 Mbinu za Kukusanyia Data

Ukusanyaji data utawezeshwa kupitia mbinu ya mahojiano na usikilizaji wa matamshi. Mbinu hizi zitatumwa kuwahoji wazungumzaji asilia wa lugha ya Ekegusii. Data kutoka mazungumzo na mijadala itanukuliwa katika maandishi ya kawaida na ya kifonetiki tayari kwa kuchanganuliwa. Matokeo yataripotiwa kwa njia ya kimaelezo.

1.8.5.1 Mahojiano

Mahojiano ni mbinu ya kupata data kupitia kwa mawasiliano ya ana kwa ana kati ya mtafiti na walengwa. Hii ni njia moja ambapo mtafiti hubadilishana nafasi na walengwa. Mtafiti atawahoji walengwa kwa kutumia maswali mseto. Katika hali hii, walengwa wataweza kujibu maswali waliyoulizwa na kujieleza au kufafanua jibu lake kadri anavyopenda. Maswali haya ndiyo yatamwezesha mtafiti kuchanganua data yake.

1.8.5.2 Usikilizaji wa Matamshi

Mbinu hii humwezesha mtafiti kutumia hisi zake zote kuelewa tajriba za walengwa na yote yanayohusu utafiti wake. Hii ni mbinu ya haraka lakini ambayo haitumiki wakati mtafiti anahitaji maelezo ya kina. Mtafiti hupata habari jinsi ilivyo kuliko kuambiwa na walengwa. Mtafiti atasikiliza kwa makini sauti za wahojiwa akiwa anarekodi kwa daftari na kwa kutumia kinasa sauti kunasa sauti za wahojiwa. Mbinu hii itatumwa kwa maana matamshi yatahitaji mzungumzaji

ambaye pia ni mwenyeji wa lugha husika. Kulingana na Chomsky na Halle (1968), wasemaji wa lugha huwa na ufahamu wa kanuni zinazoongoza matumizi ya lugha hiyo. Lengo la mbinu hii ni kupata data itakayobaini sauti ghuna na zisoghuna. Aidha, itadhihirisha mifano ya kisinkronia inayoonyesha usigano katika lugha ya Ekegusii. Data itakayokusanywa itarekodiwa tayari kuchanganuliwa.

1.8.6 Uchanganuzi wa Data

Utafiti huu utaweka pamoja data itakayokusanywa kutoka kwa walengwa na ile itakayopatikana maktabani ili kuangalia na kutathmini usawa na unukuzi wa maandishi. Data itanukuliwa kifonetiki kisha kuiainisha kulingana na sauti ili kutofautisha sauti zilizogeuzwa. Uchanganuzi huu utaongozwa na mihimili ya nadharia ya Umbo Upeo ili kutimiza malengo ya utafiti. Baada ya kuchanganua data, uwasilishaji wa matokeo utatekelezwa kwa maelezo, majedwali na vielelezo.

1.8.7 Uwasilishaji wa Matokeo

Kimsingi, muundo wa utafiti huu pamoja na uwasilishaji wa matokeo ni wa maelezo. Uchoraji na vielelezo vya majedwali utahusishwa. Uwasilisho wa aina hii unalenga kurahisisha kueleweka kwa kanuni ya Dahl inavyojidhihirisha katika lugha ya Ekegusii.

1.9 Hitimisho

Sura hii imeeleza kiini cha utafiti na utaratibu utakaozingatiwa katika kufanikisha utafiti huu. Aidha, sehemu hii imetoa usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti, mipaka na upeo, sababu za kuchagua mada, misingi ya nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada pamoja na mbinu za utafiti zitakazotumiwa.

SURA YA PILI

KANUNI YA DAHL KATIKA NOMINO NA VITENZI

2.0 Utangulizi

Sura hii inahusika na mambo mawili makuu. Kwanza, inatoa maelezo kuhusu vipengele muhimu vya kifonolojia katika lugha hii. Pili, inafanya uchanganuzi wa udhihirikaji wa Kanuni ya Dahl katika nomino na vitenzi vya lugha ya Ekegusii. Kwa kutumia mashartizuizi ya uadilifu na uziada, utafiti huu unaonyesha mabadiliko ya nomino na vitenzi katika lugha ya Ekegusii yanayodhihirisha Kanuni ya Dahl. Sura hii imechanganua data inayohusu Kanuni ya Dahl kwa mujibu wa nadharia ya Umbo Upeo. Nadharia ya Umbo Upeo inadai kwamba miundo mbalimbali ya lugha hutokana na mkinzano kati ya mashartizuizi yaliyopo. Madai hayo yamekitwa katika imani kwamba tofauti zilizopo kati ya lugha ya binadamu hutokana na tofauti za uthamini wa mashartizuizi yanayohusu mpangilio wa sauti, maneno hata virai. Vigezo vya fonolojia ya Ekegusii vilivyoshughulikiwa ni pamoja na fonimu na silabi.

2.1 Fonimu za Ekegusii

Fonimu ni kitengo cha sauti yoyote ya lugha inayobainishwa kimatamshi katika maneno ya lugha lengwa (Goldsmith 1990, Grady na Williams 2005). Fonimu huwa na sauti muhimu pamoja na zile sauti zingine zinazohusiana na fonimu hiyo

na ambazo hutumiwa mahali pa fonimu hiyo katika miktadha maalum. Utaratibu mmojawapo unaotumiwa kutambua fonimu ni wa jozi finyu (Hyman 1975). Jozi finyu ni maneno mawili ya lugha moja yanayolingana kimuundo, isipokuwa sauti moja inayotamkiwa pahala sawa, na ambayo hubainisha maana za lugha hiyo.

Kwa mujibu wa nadharia ya fonolojia zalishi, lugha zote hutawaliwa na kanuni bia kijumla (Hyman 1975). Kanuni hii inashughulikia mfumo wa sauti za lugha kwa kuweka mfuatano wa sheria za kiulimwengu zinazohusisha umbo la ndani na umbo la nje la sauti. Maumbo na miundo yote ya lugha ya binadamu hutokana na umbo la ndani, ambalo hujengeka taratibu katika akili ya msemaji mzawa lugha tangu anapoanza kujifunza lugha akiwa mtoto mdogo mpaka anapopata umilisi kamilifu wa lugha yake. Maumbo ya maneno tutamkayo katika vinywa vyetu huwakilisha umbo la nje, umbo ambalo kwa kiasi kikubwa huakisi umbo la ndani. Mojawapo ya kanuni hizo inasema kwamba mifumo yote ya kifonolojia hujumuisha sauti za konsonanti na vokali. Maneno mengi katika lugha ya Ekegusii hufuata utaratibu huu.

2.1.1 Konsonanti za Ekegusii

Utafiti huu umeweka wazi mfumo wa konsonanti za Ekegusii. Konsonanti ni sauti ambazo wakati wa kuzitamka mkondo hewa wa matamshi huzuiliwa kwa namna fulani (Schane 1973 na Hyman 1975). Sauti zenye ukonsonanti hutolewa kwa uzuiaji mkali wa mkondohewa katika sehemu ya kati ya njia ya mkondohewa.

Sauti zisizo za ukonsonanti hutamkwa bila ya kuwepo uzuiaji wa mkondohewa wa namna hiyo. Aghalabu konsonanti huwa na nguvu kuliko Vokali

Lugha ya Ekegusii ina jumla ya konsonanti ishirini na moja nazo ni; /β/ m /k /g /t / r /r /s/w /ns /s /j /n /nt/ nd /mb /m /ng /ny /ch /k /ng'/nch /nk/ kama inavyoonyeshwa katika jedwali la 2.1.

Jedwali 2.1: Konsonanti za Ekegusii


fonimu	tahajia	maneno	maana
β	b	baba	bibi
m	m	mama	mama
r	r	roar	tazama
ɣ	g	genda	nenda
t	t	tora	chuna
w	w	kweba	sahau
ns	ns	inse	chini
s	s	ise	babake
j	y	oye	wake
n	n	one	wangu
nt	nt	renta	leta
nd	nd	renda	chunga
mb	mb	embori	mbuzi
m	m	emori	ndama
ŋ	ng	tenga	cheza
ɲ	ny	enyanya	nyanya
tʃ	ch	chora	okota
k	k	kora	fanya
ng'	ng'	ing'a	nipe
ntʃ	nch	enchera	njia
nk	nk	inka	kwetu

Asili: Cammenga (2002: 190-192)

Mohammed (2001) anaeleza kwamba kwa kawaida, konsonanti hutumika katika mazingira ya awali kama konsonanti sahili au kama konsonanti changamano.

Kutokana na orodha hii ya konsonanti za Ekegusii ni dhahiri kwamba konsonanti zenyewe zina maumbo mawili. Maumbo haya ni konsonanti sahili na konsonanti changamano. Konsonanti sahili hudhihirika kwa herufi moja katika tahajia ilhali konsonanti changamano huwakilisha mwambatano wa herufi mbili. Wald (1989) anatambua kwamba konsonanti nazalishi za Kibantu zinapaswa kuchukuliwa kama fonimu zinazojisimamia na wala si mchanganyiko wa nazali na vipasuo. Kwa hivyo katika Ekegusii, mb, ng, ng' ny, nch, na nd ni fonimu zinazojitegemea. Kielelezo kifuatacho ni mifano ya konsonanti sahili na changamano.

Kielelezo 2.1: Aina za Konsonanti




Katika konsonanti sahili, kistari kimoja hutumika kuonyesha uhusiano wa moja kwa moja na rusu msingi. Vistari viwili navyo hutumika katika kuunganisha rusu msingi na herufi mbili zinazounda konsonanti changamano. Ekegusii hakina baadhi ya konsonanti zinazopatikana katika lugha nyingi za Kiafrika. Baadhi ya konsonanti hizo ni pamoja na; /dh/, /th/, /v/, /p/, /f/, /j/, z/ na sh/. Lugha ya

Ekegusii huunda maneno yake kwa kufuata utaratibu wa konsonanti vokali. Baada ya kujadili konsonanti za Ekegusii utafiti huu umebainisha vokali pia.

2.1.2 Vokali za Ekegusii

Vokali ni sauti ambazo wakati wa kutolewa kwake ala za sauti huwa hazikaribiani kiasi cha kusababisha kukatizwa kwa hewa kama ilivyo katika utamkaji wa konsonanti. Sauti zenye uvokali hutolewa kwa kuuweka mkao wa kinywa katika hali ambayo haina ubanaji wa mkondohewa. Sauti hutolewa kwa ulaini pasina hewa kubanwa. Vokali za Ekegusii zimeweza kuainishwa kimsingi kwa kutumia taratibu za mwinuko na mlalo wa ulimi. Pia unaangazia pahali pa utamkaji wa vokali; iwapo ni mbele, kati au nyuma ama ni ya juu au chini. Cammenga (2002) anaeleza kwamba Ekegusii kina vokali saba nazo ni; /a/, /e/, ε/, /i/, /o/, /ɔ / na /u/. Vokali hizi zinaweza kujitokeza katika mazingira yoyote katika neno: mwanzo, kati au mwisho. Kielelezo 2.2 chaonyesha hali ya ulimi wakati wa utamkaji wa vokali za lugha ya Ekegusii; iwapo umeinuka ama umelala.

Kielelezo 2.2: Sifa za Vokali za Ekegusii



Asili: Cammenga (2002: 193)

Kutokana na usawiri wa vokali za lugha ya Ekegusii katika kielelezo 2.2 hapo juu, ni dhahiri kwamba lugha hii ina vokali tatu za mbele ambazo ni; /i/, /e/ na /ɛ/; moja ya kati /a/ na tatu za nyuma /u/, /o/ na /ɔ/. Sifa hizi za mbele, kati na nyuma zinatambua ulalo wa ulimi wa mzungumzaji wakati wa matamshi. Kutokana na mwinuko wa ulimi, lugha ya Ekegusii inadhahirisha vokali tatu za juu /i/, /e/ na /u/ na vokali za kati ambazo ni; /ɛ/, /o/na /ɔ/ vokali ya chini kabisa ni /a/. Mkao wa ulimi pia huweza kudhibiti uanishaji wa vokali kwani inabainika kwamba ulimi unaweza kusawiri maumbo mawili makuu wakati wa kutamka vokali. Maumbo mviringo na maumbo tandazi ndiyo yameweza kuafikiwa na wanafonetiki. Irabu zote za mbele hutamkwa midomo ikiwa imetandazwa ilhali zile zote za nyuma hutamkwa midomo ikiwa mviringo. Sifa hizi za vokali hutumika kuelezea miundo tofauti ya lugha. Vokali pia zinaweza kusawiri maumbo mbalimbali ya sauti.


Jedwali la 2.2 linaonyesha maumbo mbalimbali ya vokali katika lugha ya Ekegusii.

Jedwali 2.2: Kutambua Vokali

Fonimu	Tahajia	Maneno	Maana
/a/	a	Aba	Hawa
/e/	e	Eba	Sahau
/ɛ/	e	Enda	Chawa
/i/	i	Iba	Iba
/o/	o	Oigwe	Sikia
/ɔ/	o	Ito	Wetu
/u/	u	Ura	Nyanganya

Kwa njia inayolingana na konsonanti, vokali pia hudhihirisha maumbo mawili: vokali sahili na vokali changamano. Vokali sahili ni kama vokali /i/ na vokali changamano ni mseto wa sauti sahili mbili zenye muundo sawa wa kifonetiki kwa mfano, vokali /a:/ na /ɔ:/.

Kielelezo 2.3: Vokali Sahili



Katika lugha ya Ekegusii kuna vokali fupi na vokali ndefu. Ifuatayo ni mifano ya maneno yanayotumia vokali ndefu;

8) Fupi	Kiswahili	ndefu	Kiswahili
Sik-a	heshimu	siik-a	tayarisha pombe
Tem-a	piga	teem-a	jaribu

Vokali hizi huwa huru kama vokali sahili yaani hazifungwi na mazingira ya kifonetiki. Vokali changamano ni mseto wa vokali mbili sahili zenye muundo tofauti na ambazo hutamkwa sawa na kipashio kimoja cha fonimu. Wakati vokali ya chini /a/ inaungana na vokali /u/ au /i/ huunda irabuunganifu. Hizi ni irabu mbili zinazotamkwa kwa kuunganishwa. Mifano ifuatayo ni maneno yanayotumia irabu unganifu.


9) Ekegusii	Vokali	Kiswahili
ama-iga	ai	maviga
ama-uga	au	mifupa

Uchanganuzi wa fonimu za Ekegusii umetudhihirishia kuwa vokali na konsonanti kwa jumla huchukua maumbo na miundo tofauti ingawa yana ulinganifu. Uhusiano wa vokali na konsonanti utazidi kujitokeza katika uchanganuzi ufuatao wa ruwaza za sauti katika silabi. Sauti hizi zitachangia katika utafiti huu kwa sababu ni vipashio hivi vya lugha ya Ekegusii vinavyobadilika ili kudhihirisha Kanuni ya Dahl.

2.2 Silabi za Ekegusii

Silabi ni kipashio cha kifonolojia ambacho kwa ukubwa kipo kati ya fonimu na neno (Mgullu 2001). Kwa kawaida, silabi hujumuisha kiungo cha vokali moja. Silabi hutumika kuelezea muundo wa lugha hasa kwa kiwango cha fonolojia arudhi. Vokali husika inatumiwa ikiwa kilele cha silabi (Habwe na Karanja 2004). Lugha ya Ekegusii inategemea umbo bia la silabi yaani, silabi wazi ya konsonanti–vokali (KV). Silabi wazi ni zile silabi ambazo huishia na irabu. Inaaminika kuwa matamshi ya irabu huwa hayakatiki kwa haraka kama yale ya konsonanti na kwa hali kama hiyo silabi wazi huonekana kama ipo huru au wazi zaidi. Silabi huwa na muundo wa ndani ambao ni; mwanzo na kina ambapo kina kinagawanywa tena katika kiini na koda kama inavyoonyeshwa katika kielelezo cha 2.4.

Kielelezo 2.4: Muundo wa Silabi



Maelezo haya yamesawiri uhusiano baina ya konsonanti na vokali katika kiwango cha fonimu. Silabi hutegemea lugha inayohusika na huweza kuwa sauti moja, sauti mbili au zaidi. Ni dhahiri kuwa kila lugha ina muundo wake wa silabi. Kwa kutumia nadharia ya Umbo Upeo, utafiti huu unaonyesha mabadiliko ya kanuni ya Dahl katika vitenzi pamoja na nomino. Makundi haya ya maneno katika lugha ya Ekegusii hujengeka kutokana na miundo mbalimbali ya silabi. Kwa hivyo, silabi ina mchango muhimu katika kazi hii.

2.3 Nomino za Ekegusii

Nomino ni maneno ambayo hutaja majina ya watu, vitu, mahali, vyeo, dhana na hata vitendo (Nkwera 1978 na Kapinga 1983). Nomino ni muhimu sana kwa kuwa ni lazima kila sentensi iwe na nomino au kiambishi kinachochukua nafasi ya hiyo nomino. Kuna aina mbalimbali za nomino; nomino za pekee, nomino za jamii, nomino za kawaida, nomino dhahania, nomino zinazohesabika na zisizohesabika.

2.3.1 Mofolojia ya Nomino za Ekegusii

Umbo la kimofolojia la nomino za Ekegusii huangazia viambajengo vya kimofolojia. Hivi ni vipashio ambavyo hushirikiana na vipashio vingine katika kukamilisha muundo wa kipashio kikubwa zaidi katika utaratibu wa kidaraja. Nomino ya Ekegusii ina viambishi vitatu vilivyofungamanishwa na mzizi wake:

kisabiki kiambishi awali, kiambishi awali na kiambishi tamati kama inavyoonyeshwa katika kielelezo hiki.

Kielelezo 2.5: Muundo wa Nomino za Ekegusii

O-	mo-	mura (mvulana)
Kisabiki kiambishi awali	Kiambishi awali	Mzizi

Viambishi awali huja kabla ya mzizi ilhali vya tamati huja baada ya mzizi na vyote hushirikiana kuwasilisha maana. Kiambishi awali huwezesha mzizi kuwa nomino kwa kuipa sifa za kimofolojia za idadi au ngeli. Viambishi hivi huwa ni viainisho tofauti labda vya idadi au ngeli. Kisabiki kiambishi awali pamoja na kiambishi awali huweza kubadilika kutoka kwa umoja na kwa wingi kutegemea nomino za ngeli husika.

Nomino za Kiswahili, sawa na nomino zote za Kibantu huwa zimepangwa katika ngeli au makundi tofauti. Ngeli ni utaratibu wa taaluma ya sarufi ya lugha katika kupanga aina za nomino za Kibantu (Massamba 2010). Nomino za ngeli moja hutumia viambishi vinavyofanana kwenye sentensi ili kuleta upatanisho wa kisarufi.

2.3.2 Ngeli katika lugha ya Ekegusii

Lugha ya Ekegusii ikiwa lugha ya Kibantu imeanisha nomino zake katika ngeli kwa kutumia tipolojia ya lugha za Kibantu. Mfumo huu wa uainishaji umeegemezwa sana kwenye umoja na wingi wa viambishi awali vilivyofungamanishwa na mzizi wa nomino. Cammenga (2002) ameanisha nomino za lugha ya Ekegusii katika ngeli kumi na saba. Ngeli zilizoainishwa hapa ni za nomino zinazohesabika na zisizohesabika kama inavyorejelewa katika Jedwali la 2.3.

Jedwali 2.3: Orodha ya ngeli za Ekegusii

Namba	kiambishi cha ngeli	Mfano wa nomino	Maana
1	omo-	Omonto	Mtu
2	aba-	Abanto	Watu
3	omo-	Omote	Mti
4	eme-	Emete	Miti
7	eke	Egesusu	Sungura
8	ebi	Ebisusu	Sungura
9	oro-	Orobago	Ua
10	chi-	Chimbago	Ua
10	e-	Endo	Samba
11	ch-	Chiindo	Samba
12	aka-	Akaibi	Kajizi
8	ebi-	Ebiibi	Vijizi
14	obo-	Obongo	Ubongo
6	ama-	Amango	Ubongo
15	oko-	Okogoro	Mguu
6	ama-	Amagoro	Miguu
16	aa	Aiga	Hapa
17	-me	Nyomba ime	Ndani ya nyumba

Asili: Cammenga (2002: 198-200)

Ngeli hizi kumi na saba za Ekegusii zimegawanywa kulingana na namna zinavyojitokeza (kisemantiki) na jinsi zinavyohesabika (kimofolojia). Uainishaji huu wa ngeli za Ekegusii kimofolojia ni wa maana kwetu kwa sababu, unaangazia umoja na wingi wa viambishi awali ambavyo vinatumika kuonyesha mabadiliko ya Kanuni ya Dahl. Aidha, ngeli ya kumi na tano ni ya manufaa makubwa kwa huu utafiti kwa kuwa inahusika na vitenzi visoukomo. Kitenzi kisoukomo ni umbo la kitenzi lionyeshalo kutobanwa kwa tendo katika hali fulani maalum. Aghalabu hudhihirishwa kwa kiambishi **ku-** katika vitenzi vya Kiswahili kama: kucheza, kuimba, kulia na kadhalika. Vitenzi vya lugha ya Ekegusii huchukua kiambishi awali **ko-** ambacho hupitia utaratibu wa kanuni ya Dahl.

2.4 Kanuni ya Dahl

Kanuni ya Dahl ilipata jina kutokana na mwanzilishi wake kwa jina Edmund Dahl. Hii ni kanuni kuhusu lugha ya Kibantu ambapo ikiwa kuna mfuatano wa konsonanti mbili ghuna moja hupoteza ughuna wake, au kama kuna mfuatano wa konsonanti mbili zisoghuna zote basi moja hufanywa kuwa ghuna (*Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha 1990*). Kiambishi awali kisicho ghuna kitakuwa ghuna kama mzizi utanza kwa kipande kisicho ghuna. Kwa kawaida utaratibu huu hudhihirika sana kwa kipasuo cha kaakaa laini /k/ japo pia unahusisha sauti / t-d/ na /p-b/ katika lugha zingine. Kwa mfano;

Kanuni ya Dahl katika lugha ya Ekegusii

10) Ekegusii	Kiswahili
Ok o -gamba	kuongea
Ok o -raara	kulala
Og o -tera	kuimba
Og o -teba	kusema
Og o -kana	kukataa
Og o -saba	kuomba

Kwa kawaida maneno haya hupitia mabadiliko ili kuafikiana na Kanuni ya Dahl.
Kwa mfano;

	kabla	baadaye	maana
i)	/o- k o-kamba/	[o- k o-gamba]	kuongea
ii)	/o- g o-gera/	[o- g o-tera]	kuimba

Mifano hii inaonyesha kuwa kiambishi awali /**k**/ hufuatwa na kiambishi cha mzizi ambacho ni ghuna. Aidha, kiambishi /**g**/ hufuatwa na kiambishi kisicho ghuna kama vile [t, s, k]. Viambishi awali ghuna havifuatani na viambishi vya mzizi ghuna ni sharti mabadiliko yawepo kwa kufuatwa na kiambishi kisicho ghuna. Sharti hili lisipozingatiwa maana ya neno hupotea.

/k/ → [+ghuna] / -V [-ghuna]

Konsonanti → huwa ghuna katika



isoghuna /k/ Mazingira ya konsonanti nyingine

/o-ko- gamba/

Kanuni hii inahitaji konsonanti ya kiambishi awali kutofautiana kisauti na konsonanti ya mzizi iliyoambatishwa nayo.

Kipande cha mzizi ghuna kinahitaji kiambishi awali kisicho ghuna na kipande cha mzizi kisichoghuna kinahitaji konsonanti ya kiambishi awali kilicho ghuna (Katamba 1989).

Kanuni hii hudhihirika katika nomino nyingi za Ekegusii ambapo huwa kiambishi awali kikiwa ghuna, mzizi wa konsonanti huwa sikhuna au konsonanti ya mzizi ikiwa sikhuna kiambishi awali huwa sikhuna. Hii ni kwa sababu kanuni huhitaji viambishi hivi kutofautiana kisauti.



Baada ya kubainisha fonimu, silabi na namna Kanuni ya Dahl inavyojidhihirisha katika lugha ya Ekegusii, kinachofuata ni mashartizuizi ya Kanuni ya Dahl.

2.4.1 Mashartizuizi ya Kanuni ya Dahl

Mashartizuizi ni kanuni zizotuambia kwamba ukitaka kupata umbo fulani kwa usahihi kabisa ni lazima ufanye hili na usifanye hili. Ni muhimu kusesitiza kwamba baadhi ya sarufi huhitaji kufanya mabadiliko fulani kwenye maumboghafi ili kufanya maumbotokeo yake yakubalike kwa wasemaji wazawa wa lugha inayohusika. Hii ni sawa na kusema kwamba kuna mashartizuizi ambayo hulazimisha kuwepo kwa mahitaji fulani kwenye umbo linalozalishwa ili umbo hilo likubalike. Lakini kwa kufanya hivyo huwa limevunja mashartizuizi fulani ambayo aghalabu huwa ni hafifu. Lugha ya Ekegusii ikiwa lugha ya Kibantu, hudhihirisha Kanuni ya Dahl katika vitenzi na nomino. Kanuni hii huwa na mashartizuizi. Huwa inasisitiza kuwa ikiwa kuna mfuatano wa konsonanti

mbili ghuna moja hupoteza ughuna wake, au kama kuna mfuatano wa konsonanti mbili zisoghuna basi moja hufanywa kuwa ghuna. Kwa mfano; *Obogombe* hubadilika hadi *obokombe*. Nadharia ya Umbo Upeo hutambua familia za mashartizuizi za aina mbili: familia ya mashartizuizi ya uadilifu na familia ya uziada. Masharti haya yamejadiliwa kwa undani katika sura hii.

2.4.2 Familia ya Mashartizuizi ya Uadilifu

Familia ya mashartizuizi ya uadilifu huhitaji kwamba umbotokeo (yaani umbo la nje) kwanza liwe linakubalika katika lugha inayohusika lakini pia lifanane kwa namna fulani na umboghafi lililoingizwa. Hii ina maana kwamba mashartizuizi haya huhitajia pawepo na mshabaha baina ya maumboghafi na maumbo yanayozalishwa, yaani maumbotokeo.

Kwa kuwa nadharia ya UU inaruhusu uzalishaji wa maumbotokeo usio na ukomo, ni dhahiri kwamba maumbotokeo hayo yanaweza kuwa yanatofautiana sana na maumboghafi ambayo kwayo yameegemezwa. Ili kuzuia udhahania wa hali ya juu unaoweza kujitokeza na ili kulinda uadilifu baina ya maumboghafi na maumbotokeo, kuna nadharia ya utangamano ambayo inaweka seti ya mashartizuizi ambayo hufanya pawepo na mshabaha baina ya umboghafi na umbotokeo. Na ili hili liweze kutokea imependekezwa pawepo na seti ya mashartizuizi ya utangamano kama ifuatayo.

a) FIKI-UKO

Familia ya mashartizuizi ya utangamano huweka ukomo wa kiwango cha udhahania baina ya maumboghafi na maumbotokeo kwa kuhitajia kwamba kila kitamkwa au kipandesauti cha umboghafi pia kijitokeze katika umbotokeo. Mashartizuizi haya huzuia udondoshaji wa kitamkwa au kipandesauti chochote kilichokuwa katika umboghafi. Sharti hili lina maana kwamba umbotokeo sharti lifikie ukomo wa kukubalika. Hapa inafaa tutoe mfano ili kushadidia kile kistemwacho. Kwa mfano, kuna umboghafi ‘**obokombe**’ katika Ekegusii yaani jembe katika lugha ya Kiswahili. Kutokana na umboghafi hilo tunaweza kupata maumbotokeo: **obogombe**, **eekombe** na **obokombe**. Tunapoyachunguza maumbo haya tunapata kwamba lile la kwanza halijazingatia kanuni ya Dahl yaani, viambishi vyote ni ghuna kiambishi awali na kiambishi cha kwanza cha mzizi. Kiambishi awali **b-** kinafuatwa na kiambishi cha mzizi **g-** na vyote ni ghuna. Umbo hili limevunja shartizuizi ambalo linaisitiza kiambisha ghuna kufuatwa na kiambishi kisichoghuna. Aidha, umbo la pili limevunja sharti ambapo viambishi vyote ni isoghuna. Kiambishi awali **k-** kufuatwa na kiambishi cha mzizi **k-**. Haitakikani kuwa hivyo kwa sababu kanuni inasisitiza mfuatano wa sauti ghuna na isoghuna. Kutokana na umbo la tatu ndilo linakuwa mshindi maana halijavunja sharti lolote.

b) TEGE

Familia ya mashartizuizi ya utangamano huweka ukomo wa kiwango cha udhahania baina ya maumboghafi na maumbotokeo kwa kuhitajia kwamba kila kitamkwa au kipandesauti cha umbotokeo kitegemee sauti zilizomo pia katika umboghafi. Hapa kile kinachozingatiwa ni kwamba umbotokeo linalofikia kiwango kitakikanacho cha ukubalifu ni lile ambalo kila sehemu yake inategemea kilichomo katika umboghafi. Tuchukue mfano ule wa umboghafi ‘obokombe’. Kutokana na umboghafi hilo tunaweza kupata maumbotokeo: **ekekombe**, **obogombe** na **obokombe** maumbo haya hutofautiana tu kwa jinsi vipande sauti vinavyofuatana. Mifano hiyo ya kwanza miwili imekiuka sharti la TEGE. Umbo la mwisho ndilo halikukiuka sharti la TEGE kwani kila kitu kijitokezacho ndani mwake hutegemea kile kilichomo ndani ya umboghafi.

SHABI

Familia ya mashartizuizi ya utangamano ina seti tatu ndogo ya mashartizuizi.

SHABI-[SI]

Shartizuizi hili huzuia mabadiliko ya sifa yaani, kuwe na mshabaha wa sifa za vitamkwa baina ya maumboghafi na maumbotokeo.

SHABI-[JI]

Shartizuizi hili huzuia mabadiliko ya jinsi ya matamshi baina ya maumboghafi na maumbotokeo.

SHABI-[PA]

Shartizuizi hili huzuia mabadiliko ya mahali pa matamshi baina ya maumboghafi na maumbotokeo.

2.4.3 Familia ya Mashartizuizi ya Uziada

Ni muhimu kusisitiza kwamba baadhi ya sarufi huhitaji kufanya mabadiliko fulani kwenye maumboghafi ili kufanya maumbotokeo yake yakubalike kwa wasemaji wazawa wa lugha inayohusika. Hii ni sawa na kusema kwamba kuna mashartizuizi ambayo hulazimisha kuwepo kwa mahitaji fulani kwenye umbo linalozalishwa ili umbo hilo likubalike. Lakini kwa kufanya hivyo huwa limevunja mashartizuizi fulani ambayo aghalabu, huwa ni hafifu.

Hii ina maana kwamba familia ya mashartizuizi ya uziada huweka au huondoa ‘alama’ za uziada katika maumbo ghafi na kulifanya umbo linalohusika lifikie kilele cha ukubalifu, kwa wasemaji wazawa. Yafaa tusitize kwamba idadi ya mashartizuizi ya uziada hutofautiana toka lugha moja hadi nyingine. Ifuatayo ni mifano ya mashartizuizi ya uziada katika lugha ya Ekegusii.

KILELE

Shartizuizi hili linahitaji kwamba kila silabi iwe na kiini au kilele.

H-KODA

Shartizuizi linalozuia silabi kuishia na koda.

KYI

Shartizuizi hili linaruhusu konsonanti kufuatiwa na kiyeyusho na irabu katika silabi. Masharti haya ni muhimu kwa utafiti huu kwa sababu yanatusaidia kudhihirisha mabadiliko ya Kanuni ya Dahl katika lugha ya Ekegusii. Baada ya kufafanua Mashartizuizi ya nadharia ya Umbo Upeo kinachofuata ni uchanganuzi wa data kwa kufuata masharti hayo.

Maelezo ya masharti ya Kanuni ya Dahl.

KK+GH Konsonanti mbili ghuna

KK-GH Konsonanti mbili zisizo ghuna

K+GH K-GH Konsonanti ghuna, ikifuatwa na konsonanti isoghuna

Jedwali 2.4: Kanuni ya Dahl na Mashartizuizi

Umbo msingi /obokombe/	KK+GH	KK-GH	K+GH K-GH
a) e-ke-kombe		**	
b) o-bo-gombe	**		
☞ c) o-bo-kombe			

Data hii inaonyesha nomino za Ekegusii zinazodhihirisha mashartizuizi ya Kanuni ya Dahl. Katika jedwali hili, mshindani a) anakiuka sharti kubwa ambalo lina konsonanti mbili zisoghuna zinazofuatana. Hii peke yake inamfanya

asishinde. Mshindani b) pia anakiuka shartizuizi ambalo ni mfuatano wa konsonanti mbili ghuna. Mshindani c) hakiuki sharti lolote na hili linamfanya kuwa mshindi. Konsonanti ghuna inafuatwa na konsonanti isoghuna na hivi ndivyo kanuni inataka. Kinachofuata ni udhihirikaji wa Kanuni ya Dahl katika nomino za Ekegusii.

2.5 Kanuni ya Dahl katika Nomino za Ekegusii

Kuna makundi mawili ya nomino yanayodhihirisha Kanuni hii ya Dahl. Kundi la kwanza ni lile linaloanza na konsonanti ya kiambishi awali ghuna na kufuatwa na kiambishi cha kwanza cha mzizi kisichoghuna. Kundi la pili nalo huwa na konsonanti ya kiambishi awali kisichoghuna ikifuatwa na kiambishi cha kwanza cha mzizi ghuna. Makundi haya mawili yamejadiliwa zaidi katika utafiti huu.

2.5.1 Konsonanti ya kiambishi awali ghuna inayofuatwa na kiambishi cha kwanza cha mzizi sikhuna

Katika nomino zinazodhihirisha hali hii, ni sharti konsonanti ya kiambishi awali iwe ghuna ili kiambishi cha kwanza cha mzizi kiwe sikhuna. Hii ni athari ya konsonanti mbili zikiwa pamoja. Nomino zinazofuata huonyesha mabadiliko hayo.

11) Nomino	Maana
Obo-kombe	jembe
Obo-kima	ugali

Ni dhahiri kuwa konsonanti ya kiambishi awali ghuna huhitaji kiambishi cha kwanza cha mzizi kuwa sikhuna. Kipasuo cha mdomo /β/ huhitaji kipasuo cha kaakaa laini /k/. Jedwali la 2.5 linaonyesha mabadiliko ya Kanuni ya Dahl katika nomino za Ekegusii.

Jedwali 2.5: Muundo wa Nomino na mabadiliko ya Kanuni ya Dahl

Nomino	Kiambishi awali	Mzizi	Kiambishi ngeli	Usigano	Maana
Oroteru	oro-	-teru	oro- chi	/r/- /t/	Uteo
Oroko	oro-	-ko	oro- chi	/r/- /k/	ukuni
Okogoro	oko-	-goro	Okoko- ama	/k/- /g/	Mguu

Nomino hizi zinapobadilika kwa wingi pia hufuata utaratibu huu wa Kanuni ya Dahl. Kiambishi awali kikiwa ghuna, mzizi wake huwa sikhuna. Kuna nomino zingine katika lugha ya Ekegusii ambazo mizizi yao inianza kwa vokali. Nomino hizi pia hudhihirisha utaratibu huu wa Kanuni ya Dahl. Kwa mfano;

12) Ekegusii

Viambishi

Kiswahili

Vya ngeli

e-ki-oge

eke- ebi

kitu cha makali

e-ki-ore

eke- ebi

fuvu

e-ki-age

eke- ebi

ghala la nafaka

Kawaida neno linaloonyesha utaratibu huu mzizi wake huanza kwa konsonanti lakini pia kuna yale maneno ambayo mzizi huanza kwa vokali nayo huwezesha utaratibu huu wa Kanuni ya Dahl kutokea kama inavyodhihirishwa katika Jedwali la 2.6.

Jedwali 2.6: Mzizi wa vokali na mabadiliko ya kanuni ya Dahl

Nomino	Kiambishi awali	Mzizi	Kiambishi Ngeli	Usigano	Maana
Ekioge	Eki-	-oge	Eke- ebi	/k/- /o/	Kitu cha Makali
Ekiore	Eki--	-ore	Eke- ebi	/k/- /o/	Fuvu
Ekiage	Eki-	-age	Eke- ebi	/k/- /a/	Ghala

2.5.2 Konsonanti ya kiambishi awali sikhuna ikifuatwa na kiambishi cha kwanza cha mzizi ghuna

Katika baadhi ya maneno, konsonanti ya kiambishi awali huwa sikhuna ilhali kiambishi cha kwanza cha mzizi huwa ghuna. Tofauti hizi za vitamkwa ndizo huleta mabadiliko ya Kanuni ya Dahl.

13) Sauti	Viambishi vya ngeli	Nomino	Maana
/k-b/	eke- ebi	e-ke-beya	koroboi
	eke- ebi	e-ke-boko	kiboko
	oko- ama	o-ko-boko	mkono
/k-b/	oko-ama	o-ko-goro	mguu
	eke- ebi	e-ke-genga	kipande cha ukuni

/k-r/ eke- ebi e-ke-rogo kiti

Mifano hii imezingatia utaratibu wa kanuni haijakiuka sharti la kiambishi awali na kiambishi cha mzizi. Ikiwa kiambishi awali ni ghuna kile cha mzizi lazima kiwe sikhuna. Mfano:

Kabla	baadaye	Maana
/o-ko-koro/	[o-ko-goro]	mguu
/e-ke-keya/	[e-ke-beja]	koroboi

Nomino hizi zinaonyesha kuwa hakuna maana inawasilishwa kama konsonanti mbili zisoghuna zinapofuatana. Aidha, zilizo ghuna zinapofuatana hazileti maana kabisa. Data hii yaonyesha ukweli kuwa kanuni hii hudhihirika katika nomino za Ekegusii. Konsonanti ya awali ikiwa sikhuna konsonanti ya mzizi lazima iwa ghuna ili kuthibitisha ukweli wa kanuni hii.

Upangaji wa nomino pia katika makundi ya ngeli hudhihirisha mifanyiko hii ya Kanuni ya Dahl. Kuna makundi yanayodhihirisha ukweli huu: kiambishi awali kwa umoja kikiwa na sauti ghuna, kiambishi awali kwa wingi huwa na sauti sikhuna kama inavyodhihirika katika mifano iliyo katika Jedwali 2.7.

Jedwali 2.7: Viambishi ngeli vinavyodhihirisha Kanuni ya Dahl

Namba ya Ngeli	Viambishi Ngeli	Nomino	Maana
7- 8	Eke- ebi	Ekebe	Dhambi
12- 8	Aka- ebi	Akaanga	Kaguo
15- 6	Ok- ama	Okogoro	Mguu

Viambishi hivi vya ngeli vinapobadilika kutoka kwa umoja kwenda kwa wingi huonyesha utaratibu huu wa Kanuni ya Dahl. Kwa mfano;

14) Umoja	Wingi
Eke-	ebi
Ok-	ama

Utaratibu huu haupatikani kwa makundi yote ya ngeli bali kwa mifano michache.

Kanuni ya Dahl inaweza kuchanganuliwa kwa kutumia masharti mbalimbali ya nadharia ya Umbo Upeo. Masharti hayo ni kama yafuatayo; FIKI-UKO, SHABI-(JI), PATANA, na SHABI- (SI). Masharti haya huthibitisha udhihirikaji wa Kanuni ya Dahl katika lugha ya Ekegusii. Nadharia ya Umbo Upeo ina mashartizuizi mengi lakini tumechagua machache. Miongoni mwa yale masharti machache ni haya yafuatayo;

FIKI- UKO (Fikia ukomo) Sharti hili huweka ukomo wa kiwango cha udhahania baina ya maumboghafi na maumbotokeo kwa kuhitaji kwamba kila kitamkwa au kipande sauti cha

umboghafi pia kijitokeze katika umbotokeo. Shartizuizi hili huzuia udondoshaji wa kitamkwa au kipande sauti chochote kilickokuwa katika umboghafi.

SHABI- (JI) Shartizuizi hili huzuia mabadiliko ya jinsi ya matamshi baina ya maumboghafi na maumbotokeo.

PATANA Konsonanti ya kiambishi awali ikiwa ghuna ni sharti ifuatane na konsonanti ya mzizi ambayo ni sikhuna. Aidha, konsonanti ya kiambishi awali ikiwa sikhuna basi ya mzizi sharti iwe ghuna ndio umboghafi likubaliane na umbotokeo.

SHABI- (SI) Shartizuizi hili huzuia mabadiliko ya sifa yaani, kuwe na mshabaha wa sifa za vitamkwa baina ya maumboghafi na maumbotokeo.

Jedwali lifuatalo linatumika kudhihirisha mashartizuizi ya nadharia ya Umbo Upeo kwa kutumia nomino katika lugha ya Ekegusii.

Jedwali 2.8: Nomino na mashartizuizi ya nadharia ya Umbo Upeo

Umbo msingi /oko- goro/	FIKI- UKO	SHABI- JI	PATANA	SHABI- SI
a) Oko- kogo	*			*
☞ b) Oko- goro				
c) Ogo- doro		*		
d) Oro- goro	*			*


Katika jedwali hili tunaona kwamba mshindani a) anakiuka shartizuizi kubwa la kwanza na sharti la nne. Ukiukaji wa masharti haya unamfanya asishinde ingawa hakiuki mashartizuizi mengine. Mshindani b) anakubaliana na masharti yote ya Kanuni ya Dahl ambapo kiambishi awali sikhuna kinafuatwa na kiambishi cha mzizi ambacho ni ghuna. Mshindani c) anakiuka sharti moja la SHABI-JI ilihali mshindani d) anakiuka masharti mawili la kwanza muhimu na la tatu. Tunapowalinganisha washindani hawa wote tunaona mshindi ni b) ambaye anapatana na masharti ya Kanuni ya Dahl. Baadhi ya nomino katika lugha ya Ekegusii hudhihirisha masharti haya ya Kanuni ya Dahl. Baada ya kuangalia mifanyiko hii katika nomino za Ekegusii kinachofuata ni udhihirikaji wa kanuni hii katika vitenzi.

2.6 Vitenzi vya Ekegusii

Kitenzi ni neno ambalo hutumika kama sehemu muhimu ya kiarifu cha sentensi. Dhima ya kitenzi ni kueleza na kuarifu jambo fulani linalohusu kiima cha sentensi (Kapinga 1983; Mgullu 1999). Kitenzi pia kinaweza kuangaliwa kama neno ambalo huarifu aina ya nomino. Kila kitenzi huwa na shina la kitenzi. Shina ni sehemu ndogo zaidi ya kitenzi ambayo ndiyo huwakilisha tendo hilo. Shina la kitenzi huambatishwa viambishi ili kutoa maana iliyokusudiwa kama vile mtendaji, mtendewa, wakati, kitendo kinachofanyika na pia kauli ya kitendo hicho.

Ekegusii ni lugha ambishi na kwa hivyo uambishaji hudhihirika katika kitenzi arifu kwa wingi ili kueleza hali mbalimbali. Aina mbalimbali ya viambishi awali na tamati huambikwa kwenye mzizi wa kitenzi kwa madhumuni ya kutoa kauli mbalimbali za kitenzi husika kama inavyoonyeshwa katika kielelezo 2.7.

Kielelezo 2.6: Muundo wa kitenzi Arifu cha Ekegusii



Kitenzi cha Ekegusii kina uwezo mkubwa wa kubeba viambishi kuliko aina zingine za maneno ya Ekegusii. Lugha ya Kiswahili inaonyesha mahusiano ya karibu na lugha ya Ekegusii katika vipengele mbalimbali. Hivi ni pamoja na taratibu za uambishaji na unyambulishaji. Katika lugha ya Kiswahili, kitenzi hiki huwa na sehemu tatu kuu: kiambishi awali, mzizi na viambishi tamati. Kielelezo kifuatacho ni muundo wa kitenzi katika lugha ya Kiswahili.

Kielelezo 2.7: Muundo wa kitenzi cha Kiswahili



Vitenzi hivi viwili vinalingana kwa namna ambavyo vinachukua viambishi na hili linathibitisha kuwa hizi zote ni lugha za Kibantu. Vitenzi hivi huchukua viambishi awali na viambishi tamati. Utafiti huu unaonyesha jinsi vitenzi vya Ekegusii vinavyodhihirisha Kanuni ya Dahl. Vitenzi vingi vinavyodhihirisha kanuni hii ni vitenzi jina.

2.7 Kanuni ya Dahl katika Vitenzi

Vitenzi vingi katika lugha hii hudhihirisha Kanuni ya Dahl jinsi ilivyo katika nomino. Mabadiliko ya Kanuni ya Dahl huletwa wazi kupitia kwa makundi haya mawili. Kundi linaloanza na konsonanti ya kiambishi awali ghuna na lile lingine

linaloanza na konsonanti ya kiambishi awali isiyoghuna. Jedwali 2.8 linaloonyesha mabadiliko ya Kanuni ya Dahl kwa kutumia vitenzi.

Jedwali 2.9: Muundo wa vitenzi na mabadiliko ya kanuni ya Dahl

Kitenzi	Kiambishi awali	Mzizi	Kiambishi ngeli	Mifanyiko	Maana
Okorina	Oko-	-rina	Oko-	/k/ -/r/	Kupanda
Okogera	Oko-	-gera	Oko-	/k -/g/	Kupima
Ogosaba	Oko-	-saba	Oko-	/g/-/s/	Kuomba

Kitenzi jina kinavyobadilika huwezesha Kanuni ya Dahl kutokea ambapo kiambishi awali kisichoghuna hubadilika na kuwa ghuna.

2.7.1 Konsonanti ya kiambishi awali ghuna na kiambishi cha kwanza cha mzizi sikhuna

Vitenzi vingi vinavyodhihirisha kanuni hii hutofautiana kisauti. Ikiwa konsonanti ya kiambishi awali ni ghuna, konsonanti ya kwanza ya mzizi huwa sikhuna.

15) Ekegusii

Kiswahili

o-go-tara

kutembea

o-go-tera

kuimba

o-go-tiana

kuapa

o-go-tora

kuchuna

o-go-tenena

kusimama

Utaratibu huu wa Kanuni ya Dahl hutokana na ukaribu wa mazingira ya kutamkia konsonanti hizi. Kipasuo cha kaakaa laini /g/ hubadilika na kuwa kipasuo cha ufizi /t/. Ifuatayo ni mifano mingine ya vitenzi inayodhihirisha mabadiliko ya Kanuni ya Dahl. Konsonanti ya kiambishi awali ikiwa ghuna kiambishi cha kwanza cha mzizi huwa sikhuna.

16) Ekegusii

Kiswahili

o-go-saba

kuomba

o-go-sera

kusambaratisha

o-go-soma

kusoma

o-go-sieka

kufunga

o-go-sionora

kuumiza

o-go-seria

kufukuza

Mifano hii inaonyesha jinsi kipasuo cha kaakaa laini /g/ hubadilika na kuwa kikwamizo cha ufizi /s/ ili kudhihirisha utaratibu wa Kanuni ya Dahl katika lugha ya Ekegusii.

2.7.2 Konsonanti ya kiambishi awali sikhuna na kiambishi cha kwanza cha mzizi ghuna

Kinyume na mifano ya awali, hapa konsonanti ya kiambishi awali ikiwa sikhuna konsonanti ya kwanza ya mzizi huwa ghuna. Utaratibu huu wa sauti ulisababishwa na konsonanti ya mzizi iliyofuata. Tofauti hizi za kisauti hazipatikani katika hali zote katika lugha ya Ekegusii. Kuna maneno mengine

ambayo hayafuati sharti hili lakini mifano ifuatayo hudhihirisha utaratibu wa Kanuni ya Dahl.

17) Ekegusii

Kiswahili

o-ko-genda	kwenda
o-ko-gera	kupima
o-ko-gona	kung'orota
o-ko-gesa	kuvuna
o-ko-goka	kufurahi
o-ko-gacha	kuweka
o-ko-gora	kununua
o-ko-gosa	kuogofia
/k-r/	

18) Ekegusii

Kiswahili

o-ko-rina	kupanda
o-ko-rera	kulia
o-ko-remia	kufariji
o-ko-rara	kulala
o-ko-ruga	kupika
o-ko-renta	kuleta

Mara nyingi Kanuni ya Dahl huleta umbo la kitenzi lisoukomo. Hili ni umbo la kitenzi lionyeshalo kutobanwa kwa tendo katika hali fulani maalum. Vitenzi vya

lugha ya Ekegusii huchukua kiambishi awali **ko** – ambacho kinapitia utaratibu wa Kanuni ya Dahl.

/k-b/

19) Ekegusii	Kiswahili
o-ko-bara	kuhesabu
o-ko-baga	kugawa
o-ko-buna	kuvunja
o-ko-bacha	kuchonga

Kutokana na mifano ya (a-c), kiambishi awali hutofautiana kisauti na kiambishi cha mzizi. Kipande cha awali cha silabi ndicho hutoa sharti hili na wala si konsonanti inayofuata. Uchanganuzi unaofuata hudhihirisha Kanuni ya Dahl na mashartizuizi.

Jedwali 2.10: Kanuni ya Dahl na mashartizuizi katika vitenzi

Umbo msingi	KK+GH	KK-GH	K+GH K-GH
Ogosaba			
a) Ogosaba		**	
b) Ogobaba	**		
c) Ogosaba			

Data hii inaonyesha kwamba vitenzi vya Ekegusii vinadhihirisha mashartizuizi ya Kanuni ya Dahl. Katika jedwali hili, mshindani a) anakiuka sharti kubwa ambalo lina konsonanti mbili zisoghuna zinafuatana. Hii peke yake inamfanya asishinde. Mshindani b) anakiuka sharti ambalo ni mfuatano wa konsonanti mbili ghuna. Mshindani c) hakiuki sharti lolote na hili linamfanya kuwa mshindi. Sharti linahitaji kwamba konsonanti ghuna ifuatwe na konsonanti isoghuna.

Jedwali 2.11: Vitenzi na mashartizuizi ya nadharia ya Umbo Upeo

Umbo msingi /ogo- tara/	HKODA	SHABI- (JI)	PATANA	SHABI- (SI)
a) ogo- gara		*		*
b) ogo- tara				
c) ogo- dara		*		*
d) ogo- tar	*!			

Mshindani a) anakiuka mashartizuizi mawili: shabi- (ji) na shabi- (si) ambayo husisitiza mshabaha wa sifa za vitamkwa baina ya maumboghafi na maumbotokeo. Mshindani b) ndiye mshindi kwa sababu anapatana na masharti yote ya Kanuni ya Dahl ambapo kiambishi awali sikhuna kinafuatwa na kiambishi cha mzizi ambacho ni ghuna. Mshindani c) anavunja sharti la pili na hili linamfanya asishinde. Mshindani d) anavunja sharti la kuishia kwa koda ambalo linazuia kitamkwa kuishia kwa konsonanti. Konsonanti ya kiambishi awali ghuna

sharti ipatane na konsonanti ya mzizi isoghuna. Sauti za nazali pia hudhihirisha ukweli huu wa Kanuni ya Dahl.

2.8 Usigano katika sauti za Nazali

Kuna usigano wakati kipasuo kisicho ghuna /k/ kinafuatwa na sauti za nazali.

Mifano ifuatayo inaonyesha usigano katika sauti za nazali.

20) Ekegusii	Kiswahili
e-ke-moni	paka
e-ke-nama	paja
e-ke-ng'ora	king'ora
e-ke-nyoro	kijiji

Data hii inadhihirisha kuwa hakuna masharti kwa kuunganisha konsonanti isoghuna na sauti za nazali. Nazali zinapoungana na kipasuo kisicho ghuna husababisha usigano. Kiambishi awali kisicho ghuna husababisha udhihirikaji wa Kanuni ya Dahl. Kwa kawaida, watafiti wengi husema kuwa kanuni hii hujidhihirisha kwa /k/ na /g/ pekee lakini katika lugha ya Ekegusii hujidhihirisha pia kwa mazingira ya sauti za nazali.

2.9 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia vigezo vya upatanisho wa fonolojia ya Ekegusii. Vigezo hivyo ni pamoja na fonimu na silabi. Fonimu ni kitengo cha sauti yoyote ya lugha

inayobainishwa katika maneno ya lugha lengwa. Lugha zote hutawaliwa na kanuni bia kijumla. Mojawapo wa kanuni hizo ni kwamba, mifumo yote ya kifonolojia hujumuisha sauti za konsonanti na vokali. Maneno mengi katika lugha ya Ekegusii hufuata utaratibu huu. Utafiti huu umebainisha aina mbalimbali za konsonanti na vokali katika lugha ya Ekegusii.

Aidha, kwa kutumia familia ya mashartizuizi ya uadilifu na uziada, utafiti huu umeonyesha mabadiliko ya nomino na vitenzi katika lugha ya Ekegusii yanayodhihirisha Kanuni ya Dahl. Kanuni hii inasisitiza kuwa, konsonanti ya kiambishi awali ikiwa ghuna kiambishi cha kwanza cha mzizi huwa sikhuna au mzizi ukiwa na konsonanti ya kwanza ghuna, konsonanti ya kiambishi awali sharti ichukue konsonanti isoghuna. Utafiti huu umedhihirisha kuwa nomino nyingi za kawaida na vitenzi jina katika lugha ya Ekegusii huwezesha kanuni hii ya Dahl kutokea. Aidha, utafiti umethibitisha hili kwa kutumia nadharia ya Umbo Upeo.

SURA YA TATU

MANENO MKOPO NA UDUNISHAJI

3.0 Utangulizi

Sura hii imeangazia utohozi fonolojia wa maneno mkopo ya Ekegusii. Utohozi fonolojia unahusu ubadilishaji wa vipengele vya lugha kopeshi na vile vya lugha inayokopa. Utafiti huu unategemea imani kwamba maneno mkopo hayana budi kutoholewa ili kuafiki vigezo bayana vya sarufi ya lugha inayokopa. Utohozi huu huchunguzwa kutegemea vigezo bayana vya kifonolojia, kimofolojia na kisemantiki (Mwihaki 1998). Mjadala wetu katika sehemu hii ulieleza aina mbalimbali za maneno mkopo yanayoweza utaratibu wa Kanuni ya Dahl kutokea. Aidha, sura hii imeonyesha maneno mkopo yanayoleta hali ya udogo katika lugha ya Ekegusii. Kimsingi, sura hii inaonyesha maneno mkopo yanayodhihirisha Kanuni ya Dahl.

3.1 Maneno mkopo

Ukopaji ni ule mchakato wa lugha (pokezi) kuhamisha kipashio kutoka lugha moja na kukiingiza katika lugha nyingine (changizi) (McMahon 1994). Maneno yaliyohamishwa huitwa maneno mkopo. Haya ni maneno yaliyotolewa lugha nyingine yakapewa matamshi ya lugha ngeni au lugha ya pili. Wakati lugha inakopa maneno kutoka lugha nyingine, maneno hayo huchukua miundo ya kifonolojia ya lugha ngeni.

Langacker (1967) anasema kwamba hakuna lugha ambayo wazungumzaji wake wamewahi kuingiliana na lugha nyingine na wakakosa kukopa chochote kutoka lugha ile. Hivi ni kumaanisha kwamba, ukopaji maneno unatokana na mtagusano wa lugha. Jamii inayotumia maneno mkopo huiga jambo moja au lingine kutoka nchi ngeni na kufikiria kwamba neno fulani hukubalika zaidi kuliko lile la lugha yao. Kulingana na Hooper (2005), moja kati ya matokeo ya mwingiliano wa kijamii na mawasiliano ni kuwepo kwa maneno mkopo katika jamii. Ukopaji huu husababisha mabadiliko. Chanzo cha mabadiliko huwa ni mahitaji ya ukuaji wa lugha kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine mtagusano wa lugha. Mtagusano wa lugha husababishwa na mahusiano ya kijamii kama vile shughuli za kibiashara au mwingiliano wa kitamaduni (Bynon 1996).

Paradis (1979) anasema kwamba, maneno yaliyokopwa hutamkwa tofauti katika lugha inayokopa (L2) kuliko jinsi yanavyotamkwa katika lugha changizi (L1). Maneno yanayoonyesha mguso yanakopwa zaidi kuliko yale yanayoonyesha udhahania. Field (1998) anaonyesha kuwa maana ya maneno yaliyo na mguso hupendelewa sana kuliko yale yanayotambulishwa kuwa ya udhahania.

Ni rahisi kwa lugha fulani kukopa maneno kuliko kuunda maneno mapya magumu ili kuweza kutajia vilivyoletwa na lugha ya mgusano (Nehru 1953). Ni bayana kwamba kuunda maneno mapya na kuyafanya yatumiwe na jamii ni jambo gumu na linachukua muda mrefu. Katika utafiti huu, ni wazi kwamba

lugha ya Ekegusii imeweza kuepuka ugumu huu wa kuunda nomino mpya za shughuli na vifaa vya ukarabati na imekopa moja kwa moja nomimo hizo kutoka kwa lugha zingine.

Bosire (1993) ametaja tu kwamba lugha ya Ekegusii imekopa kutoka lugha kadhaa lakini hakuzama katika maswala ya ukopaji. Lugha ya Ekegusii inapokopa kutoka kwa lugha ya Kiswahili. Vipashio vichache huathiriwa na maneno yanayokopwa huchukua miundo ya kifonolojia ya lugha ngeni. Wakati mwingine kipande cha lugha kopeshi huhifadhiwa na huwa vipande vya lugha pokezi. Namna jamii inavyokua na vitu vipya kuingizwa katika mazingira yao, linakuwa jambo la dharura kwa lugha hiyo kuendeleza msamiati wake ili kutimiza jukumu lake katika jamii (Njeru 1990). Ukopaji hutokea kati ya lugha changizi na lugha pokezi. Kwa jumla, lugha yoyote inaweza kuwa lugha changizi au lugha pokezi na kwa kweli lugha zote huweza kufanya dhima hizi zote. Kwa kawaida, lugha changizi imekubalika zaidi kitamaduni, kisiasa na kihadhi kuliko lugha pokezi. Kijumla, Kiingereza huwa lugha changizi lakini katika lugha za Kibantu, Kiswahili huwa ni lugha changizi kuliko lugha zingine.

Lugha nyingi za Kibantu hufanana sana na lugha ya Kiswahili. Sifa maarufu ya kisarufi katika lugha za Kibantu ni matumizi mapana ya viambishi na upangaji wa nomino katika makundi ya ngeli. Kila kundi la ngeli huonyeshwa kwa kiambishi ambacho ni sehemu ya nomino na huwa na upatanisho wa kisarufi. Wingi

huonyeshwa kwa kubadilisha kiambishi awali cha ngeli. Aidha, maneno mengi ya Kibantu huwa na silabi wazi ya konsonanti vokali (KV). Kulingana na Mgullu (2001), mofolojia ya maneno mengi huwa: KV, VKV, VKVKV, yaani inayoshirikisha KV. Kitenzi huwa na viambishi mbalimbali yaani viambishi awali na viambishi tamati. Viambishi hivi huwa na maana ya kisarufi na wala havina maana ya kileksia. Sifa hizi za lugha za Kibantu ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu zinatusaidia kuelewa ni kwa nini lugha hizi hukopana msamiati. Kwa msingi huu, utafiti wetu hauna budi kutalii mofolojia ya maneno mkopo katika lugha ya Ekegusii. Utohozi fonolojia ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu unapambanua maneno mkopo yanayodhihirisha Kanuni ya Dahl.

3.2 Maneno mkopo ya Ekegusii na Kanuni ya Dahl

Sarufi bia ambayo huchunguza vipengele vilivyomo katika lugha huwa na fungu la mashartizuizi ambayo sarufi ya lugha hujengeka. Kulingana na jinsi kila lugha inavyoyazingatia masharti haya ndipo kunazuka tofauti hasa lugha inapokopa msamiati wake kutoka lugha nyingine. Lugha ya Kiswahili imetumika sana kama lugha changizi katika lugha nyingi za Kibantu. Maneno mengi yanapokopwa mengine hudhihirisha kanuni ya Dahl. Kiambishi /g/ kutoka lugha ya Ekegusii kinapokopwa hubadilika na kuwa /k/ katika lugha ya Kiswahili. Kuna mifano mbalimbali inayodhihirisha ukweli huu katika lugha ya Ekegusii. Usigano katika lugha ya Ekegusii hubadilisha konsonanti ya kwanza na kuifanya ghuna kulingana

na mahitaji ya konsonanti jirani. Ifuatayo ni mifano ya maneno mkopo yanayodhihirisha Kanuni ya Dahl.

21) Kiswahili	Eke-gusii
kitanda	ege-tanda
kikapu	ege-kabu
kitabu	ege-tabu
soksi	e-so-gisi
pete	e-beta
keki	ege-ki

Maneno haya ya mkopo yanaweza kupangwa kulingana na ngeli kwa jinsi ambavyo yanadhihirisha Kanuni ya Dahl. Lugha ya Ekegusii inazo ngeli kumi na saba (Angalia Jedwali 2.3) lakini ni tatu tu zinazodhihirisha utaratibu huu maneno yanapokopwa kutoka lugha ya Kiswahili. Maneno haya yanaweza kupangwa kulingana na ngeli kama ifuatavyo;

3.2.1 Ngeli ya 12 (udogo)

Katika lugha ya Ekegusii kuna nomino zingine ambazo hazijakopwa lakini zinadhihirisha hali ya udogo. Nomino hizo ni kama zifuatazo;

22) Ekegusii**Kiswahili**

Wastani	kudunisha	Wastani	Udogo
esese	a-ga – sese	mbwa	kijibwa
engo – ko	aka – goko	kuku	kikuku
enchera	aga –nchera	njia	kijia

Kiambishi awali **ga** – na **ka** – huleta dhana ya udogo katika lugha ya Ekegusii.

Viambishi hivi vinapotumiwa pamoja na vikwamizo hudhihirisha Kanuni ya Dahl.

Watafiti wengine kama Davy na Nurse (1982) wanasema kuwa sauti zifuatazo /p, ns, nc, s, t na k/ zikiwa kwenye mzizi wa nomino huwezesha Kanuni ya Dahl katika udogo kufanya kazi kama vile;

23) Ekegusii**Kiswahili**

aga-pigipigi	pikipiki ndogo
aga-a-anto	mtu mdogo
aga-a-nse	dunia ndogo
aga-te	tawi dogo
aga-kombe	kikombe kidogo
aga-chuchu	kifaranga
aga-sese	mbwa mdogo
aga-a-nchera	njia ndogo

Mifano hii imedhihirisha matumizi ya ngeli ya kumi na mbili katika lugha ya Ekegusii katika udogo inayoleta mifanyiko ya Kanuni ya Dahl.

Nomino nyingi zinazoingia katika kundi hili huwa ni za udogo. Wakati maneno ya Kiingereza yanapokopwa kuja kwa lugha ya Kiswahili na Ekegusii vilevile, vikwamizo /f, s, sh/ huhifadhiwa. Kiambishi *aka-* hutumiwa kuonyesha udogo lakini hubadilika na kuwa *aga-* ikiwa mzizi wa neno umeanza kwa sauti sikhuna.

Kwa mfano;

24) Kiingereza	Kiswahili	Ekegusii
School	skuli	aga-sukuru
Shirt	shati	aga-shati
Radio	redio	aka-redio

Konsonanti ya mzizi ikiwa ghuna kama katika neno *radio*, konsonanti ya kiambishi awali huwa sikhuna *aka-* inayoleta dhana ya udogo. Aidha, mabadiliko haya huwezesha utaratibu wa Kanuni ya Dahl kutokea. Maneno yanapokopwa yakiwa na silabi funge lazima yatiwe vokali. Mpangilio huu wa irabu unafanywa kupitia kwa kunakili vokali au kwa kuiongeza (Kaimenyi 2002).

Jedwali 3.1: Mashartizuizi na maneno mkopo ya utohozi

Umbo msingi /ki-tambaa/	HKODA	PATANA	SHABI-(SI)	SHABI-(JI)
a) ege-gambaa			*	*
b) eke-tambaa			*	*
c) ege-tamb	*!			
☞ d) ege-tambaa				

Mshindani a) amekiuka masharti mawili ya SHABI - (SI) na SHABI- (JI) ambayo husisitiza mshabaha wa sifa za vitamkwa baina ya maumboghafi na maumbotokeo. Mshindani b) amekiuka masharti hayo mawili muhimu ambapo kiambishi awali kisicho ghuna kinafuatwa na konsonanti ya mzizi sikhuna. Mshindani c) anakiuka sharti la kuishia kwa koda ambalo linazuia kitamkwa kuisha kwa konsonanti. Mshindani d) anakubaliana na masharti yote ya Kanuni ya Dahl ambapo kiambishi awali sikhuna kinafuatwa na kiambishi cha mzizi ambacho ni ghuna. Mashartizuizi ya uadilifu hubadili vitamkwa kutoka lugha moja hadi nyingine kutegemea uzito uliopewa masharti hayo.

Vitamkwa vinavyokopwa, umbo msingi ni sharti lifanane na umbotokeo kwa kiasi fulani yaani kila kitamkwa cha umbotokeo kitegemee sauti zilizomo pia katika umboghafi. Mfano thabiti wa mabadiliko hayo ni neno “kitambaa” linapokopwa katika lugha ya “Ekegusii”. Mfano huu huonyesha namna kiambishi

awali /k/ kinavyobadilika na kuwa /g/ kinapokopwa katika lugha ya Ekegusii. Masharti ya nadharia ya Umbo Upeo yanasisitiza kuwa ni lazima kuwe na mshabaha wa sifa za vitamkwa baina ya maumboghafi na maumbokeo.

3.2.2 Ngeli ya 7/8

Hii ni ngeli ya *eke- ebi* katika lugha ya Ekegusii na ngeli ya *ki- vi* katika lugha ya Kiswahili. Ngeli hii hushirikisha maneno yanayotajia mavazi na vyombo vya nyumbani. Maneno hayo ni kama vile; *egekombe, egetambaa, egetanda, egechiko, ekerasi* na kadhalika. Sababu moja iliyowafanya wataalamu wa lugha kukopa msamiati unaotajia vyombo vya jikoni ni kuwa, nyumba ile ya kiasili ya msonge ilikuwa na vifaa vya samani vichache mno na hata nyumba zingine hazikuwa navyo. Nyumba hizi zilikuwa na mazulia makuukuu, viti vya mbao, vyungu, na sahani za mbao. Maneno mkopo katika kitengo hiki huashiria vifaa vya kisasa vilivyoletwa na wageni basi wanalugha wakaona njia moja ya kuelezea dhana hizi ngeni ni kukopa kutoka lugha ya Kiswahili.

Kiambishi awali katika Ekegusii kikiwa ghuna kinapokopwa kwa lugha ya Kiswahili hubadilika na kuwa sikhuna. Kwa mfano; *ege-kombe* hubadilika na kuwa *ki-kombe* katika lugha ya Kiswahili. Wakati mwingine kipande kile cha lugha ngeni huhifadhiwa na kuwa kipande cha lugha inayokopa. Kiambishi cha ngeli ya saba ni *eke-* lakini hubadilika na kuwa *ege-* ikiwa mzizi umeanza na sauti sikhuna. Mabadiliko haya ya viambishi vya ngeli hudhihirisha utaratibu huu wa

Kanuni ya Dahl. Jedwali 3.2 linaonyesha ukweli huu kwa kutumia mashartizuizi ya nadharia ya Umbo Upeo.

Jedwali 3.2: Maneno Mkopo na Mashartizuizi ya Nadharia ya Umbo Upeo

Umo msingi /ege-kombe/	FIKI-UKOMO	PATANA	SHABI- JI	SHABI-SI
a) Gi-gombe	*			*
b) Ki-gombe			*	
c) ki-kombe				

Katika jedwali hili tunaona kwamba mshindani a) anakiuka shartizuizi kubwa la kwanza na la nne. Ukiukaji wa masharti haya unamfanya asishinde. Aidha, mshindani b) anakiuka sharti moja la shabi-ji na hili linamfanya asishinde. Mshindani c) anakubaliana na masharti yote ya Kanuni ya Dahl ambapo kiambishi awali katika Ekegusii kikiwa ghuna kinapokopwa katika lugha ya Kiswahili huwa sighuna.

3.2.3 Ngeli ya 10/11

Maneno mengine yaliyokopwa kutoka Kiswahili hadi Ekegusii ni haya: *ebeta*, *esogisi*, *egeki* na kadhalika. Maneno haya yapo katika ngeli ya *i-zi* katika Kiswahili lakini huingizwa katika ngeli ya *e-chi* katika Ekegusii. Kulingana na hii mifano michache ni ishara tosha kwamba maneno mengine ni ya mapambo, mavazi na vyakula. Kabla ya kuja kwa wageni katika upwa wa Afrika

Mashariki Waafrika walikuwa wanatumia mavazi yao ya kiasili kama vile ngozi za wanyama na matawi ya miti. Maneno mengi yamekopwa ili kuelezea dhana hizi za kigeni lakini mifano hii tuliyotumia katika utafiti wetu ni ile tu inayodhihirisha Kanuni ya Dahl. Wakati mwingine Kanuni ya Dahl yaweza kutokea si kati ya kiambishi na mzizi tu bali pia kwenye mzizi wenyewe na katikati mwa neno kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo;

25) Ekegusii	Kiswahili
---------------------	------------------

e- sogisi	soksi
omo-gati	mkate
omo-gebe	mkebe

Maneno haya huonyesha viambishi vya mzizi vinavyobadilika ili kuonyesha ukweli huu wa kanuni. Kiambishi /g/ cha mzizi wa neno katika lugha ya Ekegusii kinapokopwa hubadilika na kuwa /k/ katika lugha ya Kiswahili. Kutokana na mifano hii kuna utohozi wa kimofolojia wa uchopezi na udondoshaji.

3.6 Hitimisho

Sura hii imechunguza utohozi fonolojia wa maneno mkopo katika lugha ya Ekegusii. Huu ni ubadilishaji wa vipengele vya lugha kopeshi na vile vya lugha inayokopa. Utafiti uliangazia maneno mkopo katika ngeli yaliyodhihirisha Kanuni ya Dahl. Ngeli hizo ni pamoja na ngeli ya 7/8, 10/11 na ngeli ya 12 mtawaliwa katika lugha ya Ekegusii. Aidha, sura hii imeonyesha maneno mkopo yanayodhihirisha hali ya udogo yanapokopwa kuja kwa lugha ya Ekegusii.

Vitamkwa hivi vinavyokopwa ni sharti vikubaliane na masharti ya Kanuni ya Dahl. Kwa hizi sura tatu zimepita umekuwa ni uchunguzi wa kisinkronia bali katika sura hii tutashughulikia uchunguzi wa kidaikronia na tabdila ni mfano mojawapo.

SURA YA NNE
MTAZAMO WA KIDAIKRONIA NA KISINKRONIA KATIKA
EKEGUSII

4.0 Utangulizi

Sura hii imelenga kufafanua mtazamo wa kidaikronia na kisinkronia katika lugha ya Ekegusii. Lugha inaweza kuangaliwa kwa njia mbili tofauti yaani, kwa kutumia sifa za kijamii au za kimfumo. Kimfumo, lugha huwa na mpangilio maalum wa vipashio vinavyotegemeana na kukamilishana. Kijamii, lugha huchunguza uhusiano uliopo baina ya lugha na jamii. Lugha ni dhana ya kawaida katika jamii inayowasaidia wazungumzaji kuwasiliana. Uchunguzi huu unaangazia tofauti za kisinkronia na kwa kutumia kanuni mbalimbali za lugha.

Utafiti huu umeangazia vitenzi vya lugha ya Ekegusii vinavyodhihirisha Kanuni ya Dahl. Vitenzi vingi vya Ekegusii huchukua viambishi awali na viambishi tamati. Kupitia kwa tabdila na mtindo wa kutumika kwingi sura hii imeonyesha namna vitamkwa hivi vinavyobadilishana nafasi ili kudhihirisha Kanuni ya Dahl. Konsonanti ya kwanza hubadilishana nafasi na konsonanti ya mwisho kwa mfululizo wa vipandesauti katika neno.

4.1 Uchunguzi wa Kidaikronia

Tawi hili la isimu ni miongoni mwa matawi makongwe zaidi. Hii ni isimu kihistoria inayolenga kufuatilia mabadiliko ya sauti, maumbo ya maneno na maana za maneno kihistoria (*Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha 1990*). Tawi hili huchunguza zaidi mabadiliko yanayotokea katika viwango mbalimbali vya lugha fulani katika vipindi mbalimbali vya historia ya lugha hiyo. Isimu historia hudhihirisha mabadiliko ambayo huwa yametokea katika viwango vya fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki katika lugha fulani. Mabadiliko ambayo huchunguzwa ni yale mabadiliko ya kidaikronia na wala siyo yale ya kisinkronia. Msisitizo wa tawi hili ni mabadiliko yaliyotokea katika lugha fulani. Kwa mfano, katika lugha ya Kiswahili neno *oa* lilikuwa *lola* wakati fulani wa nyuma. Halafu baadaye limebadilika na kuwa *oa*. Haya ndiyo mabadiliko yanayoweza kushughulikiwa. Isimu historia kwa kawaida hufanya uchunguzi wa kidaikronia ambao ni uchunguzi unaozingatia nyakati mbalimbali za historia ya lugha fulani tangu chimbuko lake, kukua kwake hadi kufikia wakati wa sasa.

Uchanganuzi wa kidaikronia ni mada moja inayozingatiwa na wanaisimu wengi kwa sababu inachangia sana nadharia za isimu. Mtazamo huu huangalia mwanzo wa lugha ya binadamu na namna ambavyo imebadilika kutoka mifumo ya wanyama, ishara na hadi sasa sifa za lugha zinazohusiana na binadamu. Isimu kihistoria ina mizizi yake katika etimolojia ya maneno kuhusu utamaduni na

elimu ya Wayunani na Warumi. Lugha zote ulimwenguni zilichipuka kutoka kwa lugha za Kilatini na Kigriki. Mnamo karne ya kumi na tisa ndipo kulichipuka na mbinu mpya za kisayansi za kulinganisha na kulinganua kanuni mbalimbali za lugha.

Taaluma hii hujishughulisha na mabadiliko katika lugha. Uchunguzi huu hulenga kujua ni mabadiliko yepi yametokea katika lugha na kwa nini yametokea. Lugha hubadilika katika hali zote za sarufi: fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Kila wakati lugha hubadilika. Kwa kawaida lugha hubadilika kutokana na mtagusano na lugha zingine. Dhana ya kijumla inayoeleza mabadiliko haya ya lugha ni ukopaji. Kidaikronia uchunguzi huu huangalia mabadiliko ya lugha kutoka hatua moja hadi nyingine. Jambo la kimsingi katika tipolojia ya kidaikronia ni ufananisho ambapo Croft anasema;

Lugha za zamani si tofauti na lugha za kisasa kwa hivyo, uchunguzi wa hivi sasa lazima urudi kwa lugha za Wayunani na Warumi (Croft 2003:233).

Sifa za lugha huonekana kubadilika kadri muda unavyosonga na hili huathiri vipengele mbalimbali vya kisarufi kama vile fonolojia, mofolojia na sintaksia. Mabadiliko ya kisauti ni miongoni mwa maswala yanayochunguzwa katika isimu kidaikronia. Mabadiliko ya kisauti huchangia mabadiliko yote katika lugha.

Baaada ya kuangalia lugha kwa mtazamo wa kihistoria kinachofuata ni uchunguzi wa lugha kisinkronia.

4.2 Uchunguzi wa Kisinkronia

Hii ni njia ya kuchunguza isimu kwa kuzingatia vipengele vya lugha jinsi vilivyo wakati huo bila kuangalia huko nyuma vilivyokuwa. Mtazamo huu huchunguza lugha kwa wakati maalum; haurejelei matukio ya zamani ili kutathimini hali yake ya sasa bali huchunguza maumbo jinsi yalivyo. Uchunguzi huu hujifunga kwa wakati mmoja maalum kwa hivyo, huangalia lugha kama mfumo unaofanya kazi kwa wakati maalum bila kuangalia jinsi imekuzwa hadi wakati wa sasa. Wakati wa uchunguzi huwa ni wakati wa sasa au wakati uliopita lakini wakati maalum. Uchunguzi wa kisinkronia unaweza kufanywa kwa lugha ambayo imefifia kama Kilatini.

Mtazamo wa kisinkronia umekuzwa ili kuweka kanuni msingi za mfumo itikadi na viambajengo vya lugha yoyote. Mtazamo huu hujulikana kama isimu fafanuzi. Hii ni mtazamo wa kiisimu unaozingatia umuhimu wa kuchambua vipengele vya lugha. Iwapo wataalamu wataweka kanuni zinazoongoza mfumo wa fonolojia ya lugha ya Ekegusii basi hii ni uchunguzi wa kisinkronia.

Katika kuhitimisha ufafanuzi wa dhana hizi ni kusema kuwa, ufafanuzi wa lugha fulani hasa chimbuko lake ni uchunguzi wa kidaikronia lakini kwa kulinganisha na kulinganua sifa tofauti za lugha hii kwa wakati maalum hii ni uchunguzi wa

kisinkronia. Lugha zinapogusana husababisha mabadiliko ya kisauti na mabadiliko hayo huchunguzwa katika tawi la kidaikronia. Baada ya kueleza maana ya dhana hizi mbili kinachofuata ni uchunguzi wa kidaikronia.

4.3 Tabdila na nadharia ya Umbo Upeo

Huu ni utaratibu katika lugha moja ambapo sauti mbili zinabadilishana nafasi katika neno. Kulingana na Massamba (2010), huu ni mchakato ambao kwa sauti mbili zilizo jirani hubadilishana nafasi. Mfano mwepesi wa kidhahania ni kama kuwa na sauti A na B zikawa katika mfuatano huo (AB) kisha zikabadilishana nafasi na kuwa katika mfuatano wa kinyume (BA). Omar (1985) anadhihirisha ukweli huu kwa kutoa mifano kutoka lugha ya Shi-Ngazija.

26) Shi-Ngazija

Kiswahili

Nga+wa+reng+a+o

ngwaareengao

wanachukua

Ka+wa+tsi+reng+a

kwaatsireenga

hawachukui

Hapa tunaona kwamba [a] ya 'nga' na [w] ya 'wa' zinabadilishana nafasi na matokeo yake ni 'ngwa'; halikadhalika tukasema [a] ya [ka] na [wa] vimebadilishana nafasi, matokeo yake yanakuwa pia yale yale [kwa]. Vyovyote tutakavyochukulia hali hii, ukweli ni kwamba kuna kubadilishana nafasi kwa maneno ya lugha hii.

Mabadiliko haya pia hutokea katika lugha ya Ekegusii. Lugha ya Ekegusii ina maneno machache yanayobadilishana nafasi kwa mfuatano wa kinyume. Dhana hii ni ya kihistoria hasa katika lugha za Kibantu. Sauti hizi katika lugha ya Ekegusii zinapobadilishana nafasi hudhihirisha Kanuni ya Dahl. Konsonanti ya kiambishi awali ikiwa ghuna, konsonanti ya kwanza ya mzizi huwa sighuna.

27)	Ekegusii	Kiswahili
	Oko- b aga	kugawa
	Oko- g aba	kugawa

Konsonanti [b] hubadilishana nafasi na konsonanti [g] na matokeo yake ni ‘baga’. Halikadhalika konsonanti [g] hubadilishana nafasi na [b] na matokeo ni ‘gaba’. Maneno haya ni sawa kimaana lakini la kwanza linachukuliwa kuwa la awali kuliko la pili. Matumizi ya maneno haya hutegemea kizazi kiyatumiayo. Mfano huu hudhihirisha Kanuni ya Dahl ambapo vipande vya sauti vilivyo ghuna katika mfumo wa sauti hubadilishana nafasi na kuwa sighuna. Vitamkwa hivi vinapobadilishana nafasi, umbo msingi ni sharti lifanane na umbotokeo kwa kiasi fulani yaani kila kitamkwa cha umbotokeo kitegemee sauti zilizomo pia katika umboghafi. Kwa mfano;

Umboghafi- /**oko-baga**/

Umbotokeo- /**oko-baga**/

Jedwali la 4.1 linadhihirisha Kanuni ya Dahl kwa kutumia Mashartizuizi ya nadharia ya Umbo Upeo.

Jedwali 4.1: Tabdila na nadharia ya Umbo Upeo

Umbo msingi /oko-gaba/	HKODA	PATANA	SHABI- (SI)	TEGE
a) Ogo-gaba			*	*
b) oko-bag	*!		*	
☞ c) oko-baga				

Mshindani a) amekiuka masharti ya *shabi-* (*si*) na *tege* ambayo husisistiza mshabaha wa sifa za vitamkwa baina ya maumboghafi na maumbotokeo. Mshindani b) amekiuka sharti la kwanza muhimu ambalo linazuia mfuatano wa konsonanti, yaani kitamkwa kuishia konsonanti. Mshindani c) anapatana na masharti ya Kanuni ya Dahl ambapo konsonanti ya kiambishi awali isoghuna sharti ikubaliane na kiambishi cha mzizi ambacho ni ghuna. Tabdila pia hujitokeza kwa mfano huu;

28)	Tabdila	Kiswahili
	a) Maro-goba	jioni
	Mago-roba	jioni
	b) Riba-ga	ruhusa
	Riga-ba	ruhusa

Kutokana na mfano huu tunagundua kuwa vitamkwa vinavyobadilishana nafasi ni pamoja na [r] na [g] na matokeo yake ni ‘rogo’ halikadhalika [g] hubadilishana na [r] na matokeo yake ni ‘goro’ japo mfano huu haudhihirishi kanuni ya Dahl. Kutokana na mifano hii tunaweza kusema kwamba kuna kubadilishana sauti kwa maneno ya Ekegusii japo si yote. Maneno haya yote hukubalika katika jamii hii bila kuleta utata wa kimaana. Viambishi tamati pia katika vitenzi hudhihirisha utaratibu huu wa kanuni ya Dahl.

4.4 Mtindo wa kutumika kwingi wa viambishi

Lugha ya Ekegusii ikiwa lugha ambishi ina uwezo wa kuongeza viambishi katika sehemu yoyote ya vitenzi vyake. Lugha hii ina uwezo wa kujenga maana baada ya maana au sentensi baada ya nyingine kupitia kwa mtindo huu wa kutumika kwingi wa viambishi. Kwa kawaida huongeza viambishi awali na viambishi tamati. Vitenzi vinapochukua viambishi huwa na maana tofauti. Kitenzi kinaporefushwa kupitia kwa viambishi maana ya kileksia hujihusisha na mahali pa kiambishi. Maana zaidi za kisarufi huonekana mwishoni mwa vokali ya mwisho ilhali ile ya kileksia hukaribiana na mzizi wa kitenzi. Vitenzi vingine vya

Ekegusii vinapoambishwa hudhihirisha Kanuni ya Dahl. Mifano ya kutumika kwingi kwa viambishi ni ile inayochukua viambishi awali katika kitenzi. Kulingana na namna ambavyo viambishi vitaongezwa, kitenzi huwasilisha maana tofauti. Kwa mfano;

29) Ekegusii

Kiswahili

Na-ko-aka	————→	na-go-aka	alikutupiga
Na-ko-koak-ete	————→	na-go-koag-ete	nilikutupiga
Na-ko-keak-erete	————→	na-go-keak-erete	nilikukupigia
Na-ka-ra-kete	————→	na-ka-rangete	nilikaranga
Na-ko-karank-ete	————→	na-go-karang-ete	nilikukaranga
Na-ko-karank-erete	————→	na-go-karang-erete	nilikukarangia

Pindi tu vitenzi vinapoambishwa, sharti la Kanuni ya Dahl lazima lizingatiwe. Konsonanti moja ikiwa sikhuna inayofuata sharti iwe ghuna kwa mtindo huu wa kutumika kwa wingi wa viambishi. Msemaji atakayetumia mfululizo wa viambishi hivi bila kuzingatia utaratibu huu basi mawasiliano yake yatatatizika. Mashartizuizi ya nadharia ya Umbo Upeo yanasisitiza kuwa ni lazima umbo msingi lifanane na umbotokeo kwa kiasi fulani yaani kila kitamkwa cha umbotokeo kitegemee sauti zilizomo katika umboghafi. Jedwali 4.2 ni dhihirisho la jinsi mashartizuizi ya nadharia ya Umbo Upeo yanavyofanya kazi.

Jedwali 4.2: Mtindo wa kutumika kwingi na mashartizuizi

Umbo msingi /na-ko-koak-ete/	HKODA	PATANA	SHABI-SI	TEGE
a) na-go-koak-et	*!			
b) na-ko-koag-ete			*	*
c) na-go-koag-ete				

Mshindani a) amekiuka sharti la kwanza muhimu ambalo linazuia kitamkwa kuishia kwa koda yaani konsonanti. Mshindani b) amekiuka masharti mawili ya **shabi-si** na **tege** ambayo husisitiza mshabaha wa sifa za vitamkwa baina ya maumboghafi na maumbotokeo. Mshindani c) anapatana na masharti ya Kanuni ya Dahl ambayo husisitiza konsonanti ya kiambishi awali isoghuna sharti ikubaliane na kiambishi cha mzizi ambacho ni ghuna. Mtindo huu wa kutumika kwingi wa viambishi unahitaji kuzingatia masharti, kwa kufanya hivyo huiwezesha Kanuni ya Dahl kutokea. Baada ya kuonyesha namna viambishi awali vinatumika kinachofuata ni viambishi tamati.

4.5 Mashartizuizi na Kanuni ya Dahl katika viambishi tamati

Hiki ni kipengele kinachohusika na uwekaji vigezo na masharti yasiyoweza kuvunjwa na yanayoweza kuvunjwa. Vigezo ambavyo ndivyo vitumikavyo katika kuamua ni umbo lipi linafikia upeo wa ukubalifu. Mashartizuizi hufanya kazi na maumbotokeo, kwa maana huyawekea maumbo hayo mashartizuizi. Lile

umbotokeo ambalo halikuvunja sharti lolote au ambalo limevunja masharti ambayo yanaweza kuvumilika ndilo lipewalo ushindi. Kwa utaratibu wa uwekaji viambishi tamati katika vitenzi kuna yale maumbo yanayovunja masharti ya Kanuni ya Dahl na kuna yale yanatii. Jedwali lifuatalo laonyesha maomboghafi na maumbotokeo na lile umbo ambalo ni mshindi.

Jedwali 4.3: Kanuni ya Dahl na Mashartizuizi katika Viambishi tamati

Umbo msingi /ngw-a-karang-et-e/	KK+GH	KK-GH	KK+GH KK- GH
a) nk w -a-karank-et-e		**	
b) ngw-a-karang-eg-e	**		
c) ngw-a-karang-et-e			

Data hii inaonyesha kuwa vitenzi vya Ekegusii vilivyoambishwa hudhihirisha Kanuni ya Dahl. Katika Jedwali hili, mshindani a) anakiuka sharti kubwa ambalo lina konsonanti mbili zisizo ghuna zinazofuatana. Hii pekee yake inamfanya asishinde. Mshindani b) pia anakiuka sharti ambalo ni mfuatano wa konsonanti mbili ghuna. Mshindani c) hakiuki sharti lolote na hili linamfanya kuwa mshindi. Kutokana na kutii sharti hili mshindani c) anakuwa ndiye bora zaidi kuliko wengine. Kila wakati maumboghafi na maumbotokeo yanahitaji kutii sheria hizi za kisarufi.

4.6 Hitimisho

Sura hii imeonyesha maana ya kidaikronia na kisinkronia. Kidaikronia ni uchunguzi wa kihistoria unaolenga kubainisha mabadiliko ya sauti, maumbo ya maneno na maana yao kihistoria. Uchunguzi wa kisinkronia ni kuzingatia vipengele vya lugha jinsi vilivyo wakati huo bila kuangalia huko nyuma vilivyokuwa. Aidha, utafiti umeonyesha nafasi ya tabdila katika lugha ya Ekegusii ikiwa ni mfano mojawapo wa kidaikronia. Huu ni utaratibu wa ubadilishanaji sauti katika neno. Mabadiliko haya yote ni ya kisinkronia na wala si ya kidaikronia. Vitamkwa vinapobadilishana nafasi huiwezesha Kanuni ya Dahl kutokea. Vitenzi vya Ekegusii vinapochukua viambihi awali na viambishi tamati vinadhihirisha Kanuni ya Dahl. Maelezo haya yote yamewekwa wazi katika sura hii.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Katika sura zilizotangulia tumechunguza udhihirikaji wa Kanuni ya Dahl katika lugha ya Ekegusii. Sura hii imehitimisha utafiti huu kwa kutoa muhtasari wa tasnifu nzima, matokeo ya utafiti, changamoto na mapendekezo.

5.2 Muhtasari

Utafiti huu ulinuia kudhihirisha Kanuni ya Dahl katika lugha ya Ekegusii. Sura ya kwanza ni muhtasari wa jinsi utafiti ulivyofanywa. Imeshughulikia usuli wa mada, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada hii, msingi wa nadharia na njia za utafiti.

Sura ya pili imeshughulikia vigezo vya kifonolojia ya Ekegusii. Vigezo hivyo ni pamoja na fonimu na silabi. Lugha zote hutawaliwa na kanuni bia kijumla. Mojawapo wa kanuni hizo ni kwamba, mifumo yote ya kifonolojia hujumuisha sauti za konsonanti na vokali. Maneno mengi katika lugha ya Ekegusii hufuata utaratibu huu. Utafiti huu umetambua aina mbalimbali za konsonanti na vokali katika lugha ya Ekegusii. Kwa kutumia nadharia ya Umbo Upeo (UU), utafiti umeonyesha mabadiliko ya nomino na vitenzi katika lugha ya Ekegusii

yanayodhihirisha Kanuni ya Dahl. Data yetu imeonyesha ukweli huu kwa kutumia nomino na vitenzi katika lugha ya Ekegusii.

Sura ya tatu tumeonyesha namna maneno mkopo yanavyodhihirisha Kanuni ya Dahl. Lugha zinapogusana hazikosi kuathiriana. Utafiti huu umeangazia maneno mkopo katika ngeli yanayodhihirisha utaratibu huu wa Kanuni ya Dahl. Ngeli hizo ni pamoja na ngeli ya 7/8, 10/11 na ngeli ya 12 mtawaliwa. Aidha, sura hii imeonyesha vikwamizo vinavyoonyesha hali ya udunishaji kwa nomino. Kiambishi awali kikiwa ghuna kinahitaji konsonanti ya kwanza ya mzizi kuwa sikhuna.

Sura ya nne imeonyesha maana ya kidaikronia na kisinkronia. Kidaikronia ni uchunguzi wa kihistoria unaolenga kubainisha mabadiliko ya sauti, maumbo ya maneno na maana yao kihistoria. Uchunguzi wa kisinkronia ni utaratibu wa kuainisha vipengele vya lugha jinsi vilivyo wakati huo bila kuangalia huko nyuma vilivyokuwa. Sura hii pia, imeonyesha nafasi ya tabdila katika lugha ya Ekegusii. Tabdila ni ubadilishaji wa sauti katika neno. Mabadiliko haya ni ya mwelekeo mmoja, neno lingine ni la kimsingi. Vitamkwa hivi vinavyobadilishana nafasi, hudhihirisha Kanuni ya Dahl. Vipande vya sauti vilivyoghuna katika mfumo wa sauti hubadilishana nafasi na kuwa sikhuna.

Data ilikusanywa kupitia uchunguzi wa kushiriki. Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa kuchunguza vigezo vilivyobadilika pamoja na taratibu zilizotumiwa kwa

maneno yaliyoteuliwa. Data iliwasilishwa kwa maelezo na udhihirishaji wa kisayansi kama vile majedwali na vielelezo mbalimbali.

5.3 Matokeo ya Utafiti

Utafiti wetu umethibitisha udhihirikaji wa Kanuni ya Dahl katika nomino, vitenzi na maneno mkopo katika lugha ya Ekegusii. Uchanganuzi wetu ulitambua kwamba fonolojia ya Ekegusii inategemea mfumo wa konsonanti ishirini na moja na vokali saba. Mpangilio maalum wa konsonanti na vokali unamlika sifa za kifonetiki ambazo kwa kawaida huhusishwa na muundo wa fonimu, nao muundo wa fonimu unamlika sifa maalum za kifonetiki zinazosawiri muundo wa silabi za Ekegusii. Imebainika kuwa lugha ya Ekegusii ina silabi wazi ambazo zina miuundo tofauti. Kuna makundi mawili yanayodhihirisha kanuni hii ya Dahl. Kundi la kwanza ni lile linaloanza na konsonanti ya kiambishi awali ghuna na kufuatwa na kiambishi cha kwanza cha mzizi kisicho ghuna. Kundi la pili nalo huwa na konsonanti ya kiambishi awali isiyo ghuna ikifuatwa na kiambishi cha kwanza cha mzizi ghuna. Upangaji wa nomino pia katika makundi ulidhihirisha mifanyiko hii ya Kanuni ya Dahl. Viambishi vya ngeli ya (7-8), (12-8), (15-6) katika lugha ya Ekegusi hudhihirisha Kanuni hii ya Dahl. Kiambishi awali kwa umoja kikiwa na sauti ghuna, konsonanti ya kwanza ya mzizi huwa sikhuna.

Vitenzi pia vimedhihirisha Kanuni ya Dahl. Vitenzi vingi vinavyodhihirisha ukweli huu hutofautiana kisauti. Ikiwa konsonanti ya kiambishi awali ni ghuna, konsonanti ya kwanza ya mzizi huwa sighuna. Imegunduliwa kuwa vitenzi vingi visoukomo huthibitisha kanuni hii. Umbo la kitenzi lisoukomo huonyesha kutobanwa kwa tendo katika hali fulani maalum. Vitenzi vingi vya lugha ya Ekegusii huchukua kiambishi awali **ko-** ambacho kinapitia utaratibu wa Kanuni ya Dahl. Kipande cha awali cha silabi ndicho hutoa sharti hili na wala si konsonanti.

Utafiti huu umebaini maeneo mbalimbali ambapo lugha ya Ekegusii imekopa msamiati wake. Sifa moja ya maneno haya ni kuwa yaliingia katika ngeli ya KI-VI katika lugha ya Kiswahili na yakaingia katika ngeli ya EKE- EBI katika lugha ya Ekegusii. Viambishi awali **ki-** au **ku-** vinapokopwa kwa lugha ya Ekegusii hubadilika na kuwa kiambishi awali **ogo-**. Aidha, ukopaji wa vikwamizo kutoka lugha ya Kiingereza kuja kwa lugha ya Ekegusii hudhihirisha utaratibu huu wa Kanuni ya Dahl. Kiambishi awali **aga-** kinapotumiwa na nomino hizi zilizokopwa huleta hali ya udunishaji.

Uchunguzi wa lugha kidaikronia na kisinkronia umedhihirisha mabadikiko mbalimbali katika lugha. Lugha hubadilika katika hali zote za sarufi: fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Kwa kawaida lugha hubadilika kutokana na mtagusano wa lugha nyingine. Uchunguzi wetu umeonyesha udhihirikaji wa

tabdila katika lugha ya Ekegusii. Tabdila ni mchakato ambao sauti mbili zilizo jirani hubadilishana nafasi. Sauti A na B zikiwa katika mfuatano wa (AB) kisha zikabadilishana nafasi na kuwa katika mfuatano wa kinyume (BA) basi huu huwa ni mchakato wa tabdila. Imebainika kuwa mabadiliko haya yanapotokea hudhahirisha Kanuni ya Dahl.

5.4 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu umepanua matumizi ya lugha ya Ekegusii katika viwango tofauti. Data iliyotumika inaweza kutumiwa kwa utafiti wa lugha za Kiafrika badala ya kurejelea tahakiki za lugha ya Kiingereza. Aidha, maneno yaliyokusanywa yanaweza kujumulishwa katika matoleo mapya ya maandishi ya Isimu Jumulifu.

Uchunguzi huu utatumiwa kubainisha tofauti zilizopo kati ya lugha ya Ekegusii na lugha nyingine za Kibantu. Kwa hivyo data inayohusika inaweza kuchangia tawi la Isimu Linganishi katika vyo mbalimbali vya isimu. Matokeo ya utafiti yana umuhimu katika kupanua maarifa kuhusu sarufi ya Ekegusii. Kwa ujumla kazi hii itawafaa wataalamu wa lugha hasa isimu ya lugha za Kiafrika.

5.5 Changamoto

Mtafiti alipata matatizo hapa na pale. Suala la fedha za kufanyia utafiti lilimtatiza si haba. Vifaa vya utafiti alivyohitaji kama kinasa sauti vilimghalimu fedha nyingi na tajriba ya kukitumia kifaa hicho pia hakuwa nayo. Mtafiti alichukua muda

mwingi kutembelea walengwa wake ambao walimpa miadi ya kurudi tena na tena. Walengwa wengine hawakupenda kuulizwa maswali kwa sababu waliona hii ni njia moja ya kuwachunguza na kutaka kujua siri zao. Ilibidi mtafiti kuwachukua pole pole ili kupata data kutoka kwao.

5.6 Mapendekezo

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Umbo Upeo kuchunguza udhihirikaji wa Kanuni ya Dahl katika lugha ya Ekegusii. Uchunguzi huu umeonyesha udhihirikaji wa kanuni hii katika nomino, vitenzi na maneno mkopo. Kwa hivyo, kuna haja ya kufanya utafiti zaidi ili kubainisha Kanuni ya Dahl katika kategoria zingine za maneno kama vile; vielezi, vivumishi na viunganishi katika lugha ya Ekegusii.

Uchunguzi umejikita katika maneno mkopo ya Ekegusii yaliyotoka kwenye lugha ya Kiswahili. Imetajwa awali kwamba lugha ya Ekegusii imekopa maneno kutoka lugha nyingine kama vile Kiingereza na lugha nyingine za Kiafrika basi, pana haja ya kuchunguza maneno mkopo yanayodhihirisha Kanuni ya Dahl kutoka lugha nyingine.

Aidha, kuna uwezekano kwamba maneno asili ya Ekegusii yanabadilishwa kutokana na mtagusano wa lugha mbalimbali katika jamii. Utafiti wa kiulinganishi unahitajika kufanywa kuhusu udhihirikaji wa kanuni hii ukiangazia makundi mbalimbali katika jamii.

Kanuni ya Dahl hudhihirika katika lugha nyingi za Kibantu basi kuna haja ya kufanya utafiti zaidi kwa lugha nyingine za Kiafrika huku watafiti wakiangalia kategoria mbalimbali za maneno.

5.7 Hitimisho

Katika sura hii, muhtasari wa matokeo, mahitimisho na mapendekezo umefanywa. Mapendekezo yametolewa kwa nia ya kufanya na kuendeleza tafiti nyingine zaidi.

MAREJELEO

- Armstrong, L. (1967) *The Phonetic and Tonal Structure of Kikuyu*. London, Bedford.
- Bennett, W. & Sharon R. (2004) *Correspondence and Molo Dissimilation*. San Diego: University of California.
- Bennett, P. R. (2013) Dahl's Law and Thagiku. *African Languages Studies*. 8: 127-159,765.
- Bickmore, L. S. (1998) *Metathesis and Dahls Law in Ekegusii*. Unpublished M.A Dissertation. University at Albany.
- Bosire, B. M. (1993) *Ekegusii. A Comparative Study of Rogoro na Maate Dialects. M. A Thesis*. Kenyatta University.
- Bynon, T. (1996) *Historical Linguistics*. London: Macmillan.
- Cammenga, J. (2002) *The Phonology and Morphology of Ekegusii- a Bantu Language of Kenya*. Koln: Rudiger Koppe Verlag.
- Chomsky, N. & Halle, M. (1968) *The Sound Patterns of English*. New York: Harper And Row.
- Croft, W. (2003) *Typology and Universals*. CUP. Chapter 8. "Diachronic Typology" Dar-es-Salaam.
- Davy, J. & Nurse, D. (1982) Synchronic Versions of Dahl's Law: The Multiple Application of Phonological Rule. *Journal of African Languages and Linguistics*: 157-195.
- Field, F. (1998) *Borrowing and Borrowability*. PhD Thesis, University of South California.
- Goldsmith, J. A. (1990) *Autosegmental and Metrical Phonology*. Oxford: Basil Ltd.
- Grady, O. & Williams (2005) *Contemporary Linguistics. An Introductoin*. 5Th Ed. Bedford.

- Guthrie, M (1967) *Comparative Bantu: An Introduction to the Comparative and Prehistory of Bantu Languages*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Hockett, C. F. (1958) A Course in Modern Linguistics. *Language Learning*, 8 (3-4).
- Hooper, B. L. (2005) Language Borrowing and the Indices of Adaptability and Receptivity. *Intercultural Communication Studies*, xiv 2005.
- Hyman, L. M. (1975) *Phonology, Theory and Analysis*. San Francisco: Rinehart and Winston.
- Kager, R. (1991) *Optimality Theory*, New York: Cambridge University Press.
- Kanana, F. (2011) Dialect Convergence and Divergence: A Case of Chuka and Imenti. *In selected proceedings of the 40th Annual Conference on African Linguistics*, Cascadilla proceedings project.
- Kapinga, C. (1983) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Katamba, F. (1989) *An Introduction to Phonology*. Edinburgh Gate: Harlow Longman.
- Kaimenyi, A. (2002) *A Tonal Grammar of Kinyarwanda: An Autosegmental and Metrical Analysis*. Lewiston, NY: The Edwin Mellen Press.
- Kombo, D. K. & Tromp, D. (2006) *Proposal and Thesis Writing. An Introduction*. Nairobi: Pauline Publication Africa.
- Langacker, R. (1967) *Language and Its Structure: Some Fundamental Linguistic Concepts*. New York: Brace and World Inc.
- Lombardi, L. (1991) *Laryngeal Features and Laryngeal Neutralization*, Doctorate Dissertation. University of Massachusetts, Amhest.
- Massamba, D. Kihore M. & Msanjila, P. (2003) *Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA) Sekondari na Vyuo*. Dar-es-Salaam. TUKI.

- Massamba, David P. B. (2010) *Phonological Theory: History and Development*. (Revised Edition) Dar es Salaam. TUKI.
- McMahon, A. M. S (1994) *Understanding Language Change*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Meinhof, C. (1932) *Introduction to the Phonology of the Bantu Languages*. Berline: Dietrich Reimer Press.
- McCarthy, J. (2003) *A Thematic Guide to Optimality Theory*. Cambridge. Cambridge University Press.
- Mgullu, R. (2001) *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mugenda, O. M. & Mugenda A. G. (2003) *Research Methods: Quantitative and Qualitative Methods*. Nairobi Acts Press.s
- Mgullu, R. S. (1999) *The Structure of Kiswahili Sentence. A Transformational Approach*. Unpublished M. A Dissertation. University of Nairobi.
- Mohammed, M. A. (2001) *Modern Swahili Grammar*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.
- Mwihaki, A.N (1998) *Loanword Nativization. A Generative View of the Phonological Adaptation of Gikuyu Loanwords*. PH.D Dissertation. Kenyatta University.
- Nehru, J. (1953) *An Autobiography*. Bombay: Bodley Head.
- Njeru, M. D. (1990) *Lexical Expansion in Kiswahili: A Study of Strategies in Corpus Development*. Tasnifu ya uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Nkwera, F. (1978) *Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Nurse, D. & Pilipson G. (2003) *The Bantu Languages*. London: Routledge.

- Omar, A. (1985) ‘*A Phonological Analysis of Shi-Ngazija.*’ Tasnifu ya M.A. University of Dar es Salaam.
- Paradis, C. (1997) Preservation and Minimality in Loanword Adaptation. *Journal of Linguistics*, 33.
- Prince, A. & Smolensky, P. (1991) Notes on connectionism and Harmony Theory in Linguistics. *Technical Report*. University of Colorado Boulder.
- Prince, A. & Smolensky, P. (1993) *Optimality Theory: Constraint Interaction in Generative Grammar*. University of Colorado at Boulder.
- Schane, S. A (1973) *Generative Phonology*. Englewood Cliffs. Prentice Hall.
- TUKI, (1990) *Kamusi Sanifu ya Lugha na Isimu: Dar-es-Salaam*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Wa Mberia, K. (1981) *The Consonant of Kitharaka*. Unpublished M.A Dissertation. University of Nairobi.
- Wald, Benji (1989) “*Swahili and the Bantu Language*” in Comri 1989, page 991-1014.

KIAMBATISHO A: Kiongozi cha Mahojiano

Maswali ya mahojiano kwa wazungumzaji asili wa lugha ya Ekegusii. Mahojiano haya ni kubainisha udhihirikaji wa kanuni ya Dahl katika lugha ya Ekegusii kwenye nomino, vitenzi na maneno ya mkopo. Pia, kuonyesha mifanyiko ya kisinkronia kwenye maneno ya Ekegusii.

1. Umezaliwa wapi?
2. Una umri wa miaka mingapi?
3. Unafanya kazi gani?
4. Unatumia lugha ngapi katika mazungumzo yako ya kila siku?
5. Umewahi tangamana na makabila mengine mbali na kabila lako?
Mtagusano huu umeathiri vipi lugha yako ya Kwanza?
6. Lugha ya Ekegusii imekopa maneno yepi kutoka kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili?
7. Maneno haya unayatumia katika mazungumzo yako?

KIAMBATISHO B: Orodha ya maneno yaliyoonyesha udhihirikaji wa

kanuni ya Dahl

Orodha ya nomino katika lugha ya Ekegusii

/k-b/

o-ko-boko -mkono

/k-g/

o-ko-goro -mguu

/k-r/

e-ke-rogo -kiti

/r-k/

o-ro-ko -kipande cha ukuni

/b-k/

o-bo-kima -ugali

/g-t/

o-go-to -sikio

Orodha ya vitenzi

/g-k/

o-ko-genda -kwenda

o-ko-gora -kununua

o-ko-gesa -kuvuna

/k-r/

o-ko-rina -kupanda

/g-t/

o-go-tara -kutembea

Maneno mkopo

/g-k/

e-ge-kombe

e-ge-tabu

e-ge-chiko

o-mo-gati

a-ga-pigipigi

Kiswahili

-ki-kombe

-ki-tabu

-ki-jiko

-M-ka-te

-pikipiki

Kiingereza

School-

Frige-

Frizzer

Ekegusii

a-ga-sukuru

a-ga-frigi

a-ga-frizzer

Maneno ya kisinkronia**Ekegusii**

Ma-goroba

Ma-rogoba

Ri-baga

Ri-gaba

Kiswahili

jioni

jioni

ruhusa

ruhusa